# Nipashe

Jumatatu Desemba 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581892

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


UKURASA WA 7
**Hoja** ya kada CCM kuhusu kukandamiza upinzani yazua jambo kisiasa

UKURASA WA 7
**Ulega** ashtuka kusuasua miradi ya barabara Dar



UKURASA WA 9
**Polisi:** Marufuku bodaboda kubeba wanafunzi

UKURASA WA 22
**ARTETA AJITETEA KUMTOA ODEGAARD**




RIPOTI MAALUMU

# Makaburi jirani na madarasa yawagharimu wanafunzi

- **Wakati** wa maziko masomo husitishwa shuleni... *Uk.2*



Sehemu ya eneo la makaburi karibu na madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 17
**WAFUGAJI KIZIMKAZI WACHOTA MBINU MKOANI IRINGA**



## Korti ya Mafisadi yamwachia huru, jaji ashangazwa na wapelelezi

UKURASA 8

# Kamati Kuu CHADEMA yateua wagombea viti vya kina Lema

UK. 3

**MICHEZO** **MAZEMBE YAMPA KIBURI RAMOVIC** UK.24 **MAONI,** UK.6

RIPOTI MAALUMU

# Makaburi jirani na madarasa yanavyowagharimu wanafunzi

## -Wakati wa maziko masomo husitishwa shuleni

**Na Mwandishi Wetu aliyekuwa** MBINGA

MADARASA yako karibu na makaburi. Kwahiyo makaburi yako karibu na madarasa. Ni makaburi yaliyofuata shule au shule iliyofuata makaburi!

Vyovyote ilivyokuwa na iwavyo sasa, wakati wa maziko masomo shuleni husitishwa na kulazimu walimu kuungana na wanakijiji katika shughuli za maziko.

Hii ni Shule ya Msingi Lipumba, katika kata ya Kihansi Mahuka, wilayani Mbinga, mkoa wa Ruvuma. Ni shule inayomilikiwa na serikali. Namba za usajili: EM 5149. Ilianza kutoa huduma mwaka 1975, yaani miaka 49 iliyopita.

Shule hii iko umbali wa Km 18.1 kaskazini mwa mji wa Mbinga. Mtu anapoanza safari kutoka mjini Mbinga kupitia barabara ya lami ya Mtwara - Mbamba Bay, ni mwendo wa dakika 22 kwa basi.

Matatizo mengi yanakabili shule hii. Mojawapo ni madarasa kuwa jirani na makaburi ya kijiji, umbali wa hatua 15 tu kutoka kwenye madarasa.

Hii imefanya kila kinachoendelea makaburini kuwa sehemu ya kinachotendeka darasani; na hata kijamii, walimu wanaofundisha shuleni hapo - mara zote katika ujirani mwema - wamebaki kuwa washiriki hai wa matukio yote kijijini - yakiwamo maziko.

Ndani ya mazingira hayo, mwanafunzi anashirikishwa mambo ambayo hakupaswa kuhusika nayo kulingana na umri wake, yakigusa pia imani za kidini, hata kijamii.

Mwanakijiji Samuel Samuel (22), aliyehitimu shuleni hapo miaka 10 iliyopita, anaeleza uzoefu wake, kunapokuwa na maziko kwenye makaburi jirani na shule, walimu wachache hubaki shuleni kuwadhibiti wanafunzi wasipige kelele wala kuchungulia na wengine huungana na wanakijiji kwenye maziko.

Anasimulia katika mazingira hayo ya kudhibitiwa darasani, anakumbuka namna wao walivyokuwa wanapambana na walimu wao kujaribu kuona kinachoendelea makaburini, ukiwa ni mvuto utokanao na utashi wao wa kitoto.

Hatua hiyo ya walimu kwenda makaburini, inatolewa ufafanuzi na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Denis Malekano (54), anayesimulia katika dhana ya ujirani mwema, walimu ni sehemu ya wanakijiji, hivyo huwajibika kushiriki maziko, wakisitisha jukumu lao la msingi la kufundisha wanafunzi. Masomo yanapisha maziko!

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu Malekano, shule hiyo hivi sasa ina wanafunzi 451 (wasichana 229). Walimu wao ni 12 (tisa ni wa kike).

Mwanakijiji Mzee Samuel Nchimbi (61), anayejitambulisha kwa kauli "nina wajukuu 13 wanaosoma katika shule hii (wanane ni wasichana)", anachangia hoja hiyo kwa kutumia uzoefu wake wa muda mrefu, akisema:

"Kuna kipindi kunakuwa na maziko karibu kila wiki. Inakuwa kikwazo kikubwa kwa wanafunzi kwa sababu wakati wa maziko, vipindi vyote vya masomo vinasitishwa shuleni, walimu wanajumuika nasi hadi tunapokamilisha shughuli hiyo."

Mzee Nchimbi ambaye ni baba wa mhitimu wa shule hiyo, kijana Samuel, anarejea historia tangu zama walizoikaribisha shule hiyo katika kashikashi za msukumo wa Ujamaa Vijijini, akiwa na simulizi:

"Mimi nimezaliwa hapa Lipumba, nimeyakuta makaburi haya. Historia yake ni kwamba, kulikuwa na eneo lenye ukubwa wa ekari 60. Lilikuwa chini ya wamisionari. Mwaka 1975, likagawanywa -- ekari 42 zikatengwa kuwa eneo la shule ya msingi na ekari 18 zikatengwa kwa ajili ya kanisa la RC (Roman Catholic) na makaburi."

Hata hivyo, Mzee Nchimbi anabainisha kuwa mwili wa kwanza kuzikwa katika eneo hilo lililotengwa kwa ajili ya makaburi ya kijiji, ulizikwa mwaka 1932, kipindi hicho eneo likiwa chini ya wamisionari. Makaburi yalitangulia madarasa!

"Uzikaji ulikuwapo hata kabla ya kugawa eneo hili. Mtu wa kwanza kuzikwa katika makaburi haya ni Yombayomba Mpiti ambaye ni babu wa babu yangu. Huku kwa lugha yetu tunamwita "mtete".

"Eneo hili la makaburi linatumika kusitiri miili ya watu wa hapa kijijini Lipumba. Na hakuna ubaguzi; wakristo, waislamu wanazikwa hapa. Mimi mwenyewe ni Mashahidi wa Yehova, lakini nikifa nitazikwa hapa."

Mwenyekiti wa Kanisa Katholiki Lipumba, Parokia ya Kigonsera, Jimbo la Ruvuma, Augustino Msuha, anaungana na mwanakijiji mwenzake, Mzee Nchimbi kwamba madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba kuwa karibu na makaburi hayo kuna madhara kwa wanafunzi.

"Walimu wanapositisha vipindi na kuja huku makaburini kuzika ni usumbufu kwa watoto na hali hii ina madhara kitaaluma na kisaikolojia kwa wanafunzi. Msiba unamwumiza hata mtu mzima, wale watoto (wanafunzi) wanakuwa katika hali mbaya zaidi.

"Sisi (kanisa) hivi sasa hatuna uwezo wa kujenga ukuta kutenganisha makaburi na madarasa, lakini tumeamua kupanda miti mpakani mwa shule na eneo la makaburi. Miti hii ikishakua itawazuia wanafunzi kuona kinachoendelea makaburini. Watasikia nyimbo na sala za mazishi, lakini hawataona kinachojiri," anasema Mwenyekiti Msuha.



Sehemu ya eneo la makaburi karibu na madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Alipoulizwa na mwandishi wa habari hii kuhusu idadi ya waliozikwa katika makaburi hayo, Msuha (61) alitoa maelezo yafuatayo:

"Makaburi haya ni ya kijiji, lakini yako chini ya kanisa tangu miaka ya 1930. Jamii yote ya Lipumba inazikwa hapa. Ni vigumu kujua idadi ya waliozikwa hapa mpaka sasa kwa sababu uzikaji ulianza zamani mno.

"Kuna kipindi tunapochimba, tunakutana na mafuvu, maana yake ni kwamba eneo hilo ulizikwa mwili wa binadamu zamani sana. Baadhi ya makaburi yameshafutika, yanayoonekana kwa urahisi ni haya yaliyojengewa. Ni maelfu ya watu wamezikwa hapa, eneo hili la makaburi ni kubwa, ekari 18."

Wakati kukishuhudiwa hali hiyo shuleni Lipumba, Mwongozo wa Uthibiti wa Ubora wa Shule uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Juni mwaka huu, unaelekeza kufanyike tathmini yakinifu ya kimazingira, kijamii na kihisia katika muktadha wa elimu.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, uhakiki huo unapaswa kujumuisha muundo wa miundombinu na hali ya jumla ya shule. Lengo ni kuhakikisha mazingira ya shule yanakuza hali chanya, jumuishi na salama kwa ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi.

Aya ya 4:11 ya mwongozo huo inaelekeza shule na walimu hujenga mazingira rafiki kwa watoto kujifunza na kucheza kwa usalama.

Vilevile, Aya ya 38 ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (marejeo ya mwaka 2023), inaelekeza serikali ihakikishe inatengeneza mazingira salama na rafiki katika taasisi za elimu na mafunzo nchini.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lipumba, Mathias Mpangala anakiri mazingira ya sasa shuleni Lipumba, hasa katika eneo hili la makaburi kuwa jirani na madarasa, yanakinzana na sera na miongozo ya utoaji elimu nchini.

"Shule hii ni kongwe. Madarasa yake yamechakaa kiasi kwamba hayahitaji kukarabatiwa, bali kubomolewa na kujengwa upya. Kwa kutambua kwamba yalijengwa karibu na makaburi, hivi sasa madarasa mapya tunayojenga tunahakikisha yanakuwa mbali na makaburi.

"Tumekubaliana na wanakijiji kila mwaka walau tujenge darasa moja lenye vyumba viwili na ofisi ya walimu. Tayari wanakijiji wamechangia ujenzi wa darasa moja, ujenzi wake umefikia hatua nzuri, kilichobaki ni kumalizia sakafu na lipu.

"Lengo letu ifikapo mwaka 2026, tuwe na madarasa mapya manne katika shule yetu yenye vyumba viwili na ofisi moja ya walimu kwa kila darasa.

"Halmashauri nayo mwaka jana ilitupatia fedha za kujenga darasa moja, Sh. milioni 40. Ujenzi wake umefikia hatua ya kuezeka. Madarasa haya mapya yanajengwa umbali wa mita 200 kutoka mpaka wa shule na eneo la makaburi. Lengo letu madarasa yatoke kule karibu na makaburi," anasema Mpangala.

Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inaelekeza "wananchi watashiriki shughuli za serikali yao kwa mujibu wa Katiba hii". Je, wakazi wa kijiji cha Lipumba wanashiriki vipi kunusuru shule ya msingi iliyomo kijijini mwao?

Mwanakijiji Remista Ndunguru (46) anasema kuwa mwaka 2022 walikubaliana katika kikao cha kijiji wachangie Sh. 20,000 kwa kila kaya yenye mke na mume au Sh. 10,000 kwa kila kaya yenye mzazi mmoja.

Ndilo fungu ambalo Ofisa Mtendaji Mpangala anajivunia linatumika katika ujenzi unaoendelea wa darasa lenye vyumba viwili na ofisi ya walimu.

Remista anayejitambulisha ni mama wa watoto watatu wanaosoma katika shule hiyo (mmoja wa kike yuko darasa la sita na wawili wa kiume wanaosoma darasa la nne na la awali), anasema:

"Kama mzazi nina uchungu na ile hali iliyoko shuleni kwa wanangu. Muda wa kuzika, walimu wachache wanaobaki shuleni, hupita kila darasa kutoa tahadhari watoto (wanafunzi) wasipige kelele. Kunakuwa na ukimya shuleni mpaka pale maziko yanapokamilika.

"Ni hali inayowajengea woga wanafunzi. Yaani mtoto yuko darasani lakini anaogopa kinachoendelea makaburini. Hali hii inawaletee shida wanafunzi kifikra. Siku ya maziko wanafunzi ni kama hawasomi kabisa, maana kunakuwa na pitapita ya watu shuleni wanapokwenda makaburini, pia wakati wa kutoka makaburini."

Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Veronica Justine, alipotafutwa na mwandishi wa habari hii Novemba 24 mwaka huu kuzungumzia kinachojiri katika shule hiyo, alisema:

"Ninatambua changamoto zinazoikabili Shule ya Msingi Lipumba, lakini msemaji wa halmashauri ni mkurugenzi. Nikizungumzia suala hili, nitakuwa ninakiuka taratibu."

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Joseph Kashushura, alipotafutwa na mwandishi wa habari hii kuzungumzia suala hilo, alitoa ufafanuzi ufuatao:

"Nina taarifa kuhusu changamoto ya miundombinu katika shule hiyo. Nina shule za msingi 168, nyingi zilijengwa zamani, majengo yake yamechakaa kama hiyo ya Lipumba.

"Kuhusu maziko kuingilia ratiba ya vipindi shuleni, nitawasiliana na Ofisa Elimu Msingi (Veronica) ili kupata taarifa kamili ya suala hilo kabla ya kuzungumzia kwa undani."

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***

**ITAENDELEA KESHO**

## HABARI KITAIFA

# Kamati Kuu CHADEMA yateua wagombea viti vya kina Lema

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeteua wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kwa kanda mbili.

Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema si miongoni mwa wagombea wa nafasi hiyo kwa kanda hiyo.

Lema alishatangaza siku nyingi kuwa hatogombea katika nafasi hiyo huku jina lake likiwa miongoni mwa yanayotajwa huenda yakawamo katika orodha ya wanaotaka kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, uteuzi wa wagombea uongozi kwa Kanda ya Kaskazini na ya Kati, umefanywa na Kamati Kuu ya chama hicho iliyoketi Desemba 14 mwaka huu.

Wagombea walioteuliwa ni kwa nafasi za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mtunza Hazina Kanda na mabaraza.

Kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini aliyeteuliwa ni Antony Mallya, Michael Kilawila na Samweli Welwel.

Kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti, walioteuliwa ni Gervas Sulle, Elifuraha Matela na Emmanuel Landey.

Walioteuliwa kwa nafasi ya Mhazini ni Bahati Mollel na Emma Kimambo.

Kwa upande wa Baraza la Wazee, wanaogombea nafasi ya Uenyekiti ni Kidawa Iyavu na Leonard Mao wakati nafasi ya Makamu Mwenyekiti inawaniwa na mgombea mmoja, Jomba Koyi na nafasi ya Katibu wa Baraza hilo, aliyepitishwa ni Julius Sarmet.

Walioteuliwa Baraza la Wanawake kwa nafasi ya Uenyekiti ni Luisesia Ndesamburo, Makamu Mwenyekiti ni Rebeca Mngodo wakati nafasi ya Katibu ni Rachel Kiogwe, Jackline Kimabo na Mamuu Lolo na nafasi ya Mhanzini ni Zuena Mwanga.

Upande wa Baraza la Vijana, nafasi ya Uenyekiti wanaogombea ni Gasper Temba na Jakson Msoka, wakati nafasi ya Katibu ni Amani Kimath na Beda Fransis.

**KANDA YA KATI**

Kwa Kanda ya Kati, wanaogombea nafasi ya Uenyekiti Chama ni David Mghanja, Devotha Minja, Ezekiel Chisinjila, Idd Kizota na Shujaa Evarist, wakati nafasi ya Makamu Mwenyekiti wanaogombea ni Daniel Marwa, Godfrey Charles, Imelda Malley na Jingu Jackson na nafasi ya Uhazini, wanaogombea ni Honest Msaki, Kapalatu Singamagazi na Modestus Chitemi.

Upande wa Baraza la Wazee, wanaogombea ni Aquilin Magalambula, Mathew Likwina, wakati nafasi ya Makamu Mwenyekiti wanaogombea ni Ester Jingu, nafasi ya Katibu ni Paul Eugen na nafasi ya Mhazini ni Jella Mambo.

Kwa upande wa Baraza la Vijana la Kanda hiyo ya Kati, Kamati Kuu imewatea wanaogombea Silvery Dodo na Hilda Mbuli kwa nafasi ya mwenyekiti.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customer-relations@guardian.*



Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema **PICHA:MTANDAO**





Skani hapa kutembelea chaneli yetu


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 28273 YA 2024**

- **SAID RAJAB SALUM**
- **HUSNA SALUM MADABA……WADAI**

**DHIDI YA**

- **THE CITY COUNCIL OF DODOMA**
- **PAULINE BENARD MGALAH**
- **MUSSA HALIFA MOHAMED**
- **ANDREW WAZOEL MBWAMBO**
- **COMMISSIONER FOR LANDS**
- **REGISTRAR OF TITLES**
- **THE ATTORNEY GENERAL …………. WADAIWA**

**KWA: MUSSA HALIFA MOHAMED**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 28273 YA 2024**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. E. E. KAKOLAKI, JAJI wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu na dakika Arobaini na tano (3:45) asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 13/2/2025.

HIVYO BASI; unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .

NA ENDAPO; hutafika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA; Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 Desemba, 2024.

**NAIBU MSAJILI**
**DODOMA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA ARUSHA, KILIMANJARO NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHEMBA, KONDOA NA MJI WA KONDOA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dodoma katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, na Mji wa Kondoa kuanzia tarehe 11 hadi 17 Desemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 11 hadi Jumanne tarehe 17 Desemba, 2024.
2. VITUO: Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua namba 3 (Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Desemba, 2024 na:

**Livini A. Morrice**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218284201



**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**CAP 117**
**CHANGE OF NAME BY DEEP POLL**

**BY THIS DEED I, AYUB TIMOTHY BALENDWA of, DAR ES SALAAM, DO HEREB**Y wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names **AYUB TIMOTHY ELIAS BALENDWA** that appear on my birth certificate because the name"ELIAS" was mistakenly added on my birth certificate and **AYUBU TIMOTH BALENDWA** that appear on my National Identity card because the first, name and the middle name were misspelled.

As from the date of this deed poll for the purpose of evidence of such determination, I hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **AYUB TIMOTHY BALENDWA.**

**I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated describe and address me by the adopted name of A**YUB TIMOTHY BALENDWA** in substitution of my former names **AYUB TIMOTHY ELIAS BALENDWA** and **AYUBU TIMOTH BALENDWA.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have set my hand at Dar es Salaam, and I hereon substitute my old name of **AYUB TIMOTHY ELIAS BALENDWA and AYUBU TIMOTH BALENDWA** with my new name of **AYUB TIMOTHY BALENDWA.**

**SWORN** at **DAR ES SALAAM** by the said
**AYUB TIMOTHY BALENDWA**
Who is known to me Personally/Identified to me by………… the latter being known
To me personally in my presume this 18th day of October, 2021

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA. 15 MWAKA 2024**
**FADHILI EMILY**
**KABUJANJA…………..MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MVANO YUSUFU SELEMANI NA WENZAKE**
**6……………MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MVANO YUSUFU SELEMANI NA WENZAKE 6 – POPOTE MLIPO.**

**F**ahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mheshimiwa F. CHINUKU Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.


AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi 11 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **KARAMA ABDALLAH KARAMA** amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 982 DKK** aina ya **SUZUKI JIMY.** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/KIN/271865/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PENDO LAURENT MGUJI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No 0055 Kilichotolewa na baraza la mtihani wa taifa mwaka 2015 shule ya sekondari , MAJENGO MOSHI MJINI. Cheti cha Diploma ya Nursing kilichotolewa, MUHIMBILI mwaka 2019.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu naye .

**Polisi taarifa: PHQ/DAR/TEM/273700/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ROBERT ENOS MFINANGA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 341 DWQ, MC 561 DWQ na MC 368 DWP** zilizotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa yeyote atakayeziona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

**TAARIFA YA POLISI:**
**PHQ/DAR/KIG/275652/2024.**

## TANGAZO PICHA

# PICHA ZA MATUKIO YA TRA MWEZI DESEMBA 2024



MENEJA MSAIDIZI WA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) MKOA WA KIKODI WA TEGETA, BI MAI GLORIA SARIA AKISHIRIKIANA NA WATUMISHI WENGINE WA TRA TAREHE 14/12/2024 WAMEWATEMBELEA WAFANYABIASHARA WAKUBWA WA ENEO LA GOBA; B&B SPECIALIZED POLYCLINIC PAMOJA NA GAF INTERNATIONAL GROUP LIMITED KWA LENGO LA KUWASHUKURU KWA ULIPAJI KODI WAO MZURI KWA MWAKA HUU 2024, PIA KUWASIKILIZA NA KUJUA CHANGAMOTO ZAO NA KUZITATUA. SAMBAMBA NA HILO KUWASIKILIZA WAFANYABIASHARA WENGINE WA ENEO LA GOBA CENTER KWA NJIA YA MLANGO KWA MLANGO ILI KUWAWEZESHA KULIPA KODI YA MAPATO AWAMU YA NNE











## TANGAZO PICHA

# MATUKIO KATIKA PICHA ZA TRA MWEZI DESEMBA 2024



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA), MKOA WA MWANZA TAREHE 14 DESEMBA, 2024 IMEENDELEA NA ZOEZI LA KUWATEMBELEA WATEJA WAKE NA KUTOA ZAWADI ZA KRISMASI NA MWAKA MPYA KWA LENGO LA KUWASHUKURU KWA MCHANGO WAO KATIKA KUFANIKISHA MAKUSANYO YA KODI.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA), MKOA WA IRINGA TAREHE 14 DESEMBA, 2024 IMEENDELEA KUDUMISHA MAHUSIANO MAZURI NA KUWASHUKURU WAFANYABIASHARA WAKE MKOANI HAPO KWA KUENDELEA KUTIMIZA WAJIBU WAO WA KULIPA KODI KWA WAKATI.





MENEJA WA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA), MKOA WA MTWARA, BI. MAIMUNA KHATIB AKIWA AMEAMBATANA NA WATUMISHI WENGINE WA TRA TAREHE DESEMBA 14, 2024 WAMEKUTANA NA MAWAKALA WA FORODHA KUTOKA BANDARI YA MTWARA NA KUSIKILIZA CHANGAMOTO ZAO PAMOJA NA KUWASHUKURU KWA ULIPAJI WAO MZURI WA KODI. AIDHA AMEWAPONGEZA KWA USHIRIKIANO WAO MKUBWA WANAOUTOA KWA TRA.



MENEJA WA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA), MKOA WA MTWARA, BI. MAIMUNA KHATIB AKIWA AMEAMBATANA NA WATUMISHI WENGINE WA TRA TAREHE DESEMBA 14, 2024 WAMEKUTANA NA MAWAKALA WA FORODHA KUTOKA BANDARI YA MTWARA NA KUSIKILIZA CHANGAMOTO ZAO PAMOJA NA KUWASHUKURU KWA ULIPAJI WAO MZURI WA KODI. AIDHA AMEWAPONGEZA KWA USHIRIKIANO WAO MKUBWA WANAOUTOA KWA TRA.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dirisha la usajili limefunguliwa, wachezaji wa benchini amkeni

**KIPINDI** cha dirisha dogo la usajili kimefika, kila klabu ikisaka wachezaji ambao inaona watawasaidia kuongeza nguvu kwenye vikosi vyao.

Hiki ni kipindi ambacho baadhi ya wachezaji hupelekwa kwa mkopo kwenye timu zingine baada ya kuonekana kuna changamoto ya kupata namba katika vikosi walivyopo.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wachezaji hasa walio kwenye timu kubwa hukataa kutolewa kwa mkopo na badala yake wanaridhika kusugua benchi ili mradi tu mshahara wao unaingia.

Matokeo yake wanakaa hapo hadi mkataba wao unapoisha, wanaachwa na kuanza tena upya majina yao yakiwa yamepotea kwenye ramani ya soka kutokana na viwango vyao kushuka.

Hivyo, wakati huu wa kipindi cha dirisha dogo ni muda muafaka kwa wachezaji wao wenyewe kuziomba klabu zao kuwatoa kwa mkopo ili wakaboreshe viwango vyao na kuendelea kuwa wa moto.

Kuomba kutolewa kwa mkopo si kwamba uwezo wa mchezaji umeisha, ila anakwenda sehemu ambayo atapata nafasi ya kuwathibitishia waajiri wake kuwa bado ana uwezo mkubwa na kinachokosekana kwake ni nafasi ya kucheza tu.

Imeshatokea mara nyingi baadhi ya wachezaji kutolewa kwa mkopo na kurejeshwa tena kwenye klabu yake mama baada ya uwezo wake kuonekana kule alikokwenda.

Mfano mdogo ni David Kameta 'Duchu', ni miongoni mwa wachezaji ambao walisajiliwa Simba miaka kadhaa iliyopita kutoka Lipuli ya Iringa na amekuwa akitolewa mara kwa mara kwa mkopo, lakini kila anakokwenda anafanya vizuri na Simba inamrejesha na kumuongeza mkataba, halafu inamtoa tena, na sasa amerejea tena kwenye kikosi cha Simba.

Kwa sasa hapati nafasi ya kucheza, mchezaji huyo anaweza kuwaomba tena waajiri wake kumtoa kwa mkopo kwa sababu yeye mwenyewe anajua faida hiyo, huwa inamrudisha tena Simba.

Tatizo la wachezaji wengi wa Tanzania ni woga wa maisha. Wanapokuwa kwenye klabu ambazo mshahara wao ni mkubwa kidogo na wana uwezo wa kuupata kwa wakati, huwa hawapendi kujishughulisha kwenda klabu ambazo watapata nafasi ya kucheza kwa sababu tu ya kutokuwa na uhakika wa kulipwa kwa wakati, pamoja na posho kiduchu.

Yanga ina mchezaji kama Denis Nkane, Kibwana Shomari, hawa wote si wachezaji wa kikosi cha kwanza, lakini wana uwezo wa kucheza mechi zote wakienda kwenye klabu zingine zinazowahitaji.

Simba ina makipa wengi kiasi kwamba wengine hawajulikani watacheza lini, lakini huenda hakuna hata mmoja anayetaka kuondoka kwenda timu zingine.


Tukiangalia, kuna baadhi ya timu zina makipa wa viwango vya chini mno, hivyo kipa kama Aishi Manula, Hussein Abel wanaweza kuomba kuelekea kwenye timu zingine ili wapate nafasi ya muda wa kucheza kwa manufaa yao na klabu yao kwa ujumla, kwani wanaweza kuwa fiti baada ya msimu tofauti na sasa ambapo wanakaa kumuangalia, Moussa Camara akidaka na Ally Salum akiwa kipa namba mbili.

Katika kipindi hiki, klabu nazo pia zisisajili kwa mihemko, badala yake ziangalie maeneo muhimu ambako zina mapungufu tu.

Zisikubali kusajili ili mradi tu, au kulundikiwa wachezaji wa mkopo kutoka timu fulani ambao kwao hawana umuhimu nao. Hiki ni kipindi cha kupata wachezaji wachache tu ambao wataviimarisha vikosi na si kusajili kwa 'fasheni'.

Hilo likifanyika kwa umakini litaongeza pia ushindani kwenye Ligi Kuu na michuano mingine na kulifanya soka la Tanzania kuzidi kuwa na mvuto zaidi, kitu ambacho sisi kama wadau wa soka namba moja, tunatamani kukiona kikitokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# VAR Mobile ndizo zitakuwa mwarobaini wa Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwangwo

**NI** wazi kuwa msimu wa 2024/25 Ligi Kuu Tanzania Bara itamalizika bila kuwa na Teknolojia ya Video ya kumsaidia Mwamuzi, VAR.

Hii ni tofauti kabla ya kuanza msimu ambapo viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), walisema teknolojia hiyo itatumika nchini.

Mtambo wa VAR ukaletwa na kufungwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, tukaambiwa pia kuwa wadhamini wanaoonesha ligi hiyo watanunua mtambo wa VAR ambao unatembea (VAR Mobile), ambao utakuwa unakwenda popote pale nchini ambapo mechi inachezwa.

Bosi mmoja wa TFF alisema watatengeneza kanuni ambayo inafanya mechi mbili za ligi ziwe zinatumia VAR, na hasa zile zenye mvuto wa mashabiki kama za Simba na Yanga.

Alikuwa na maana kama Yanga inacheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambako kumefungwa VAR, Simba ikienda kucheza Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza basi ile VAR Mobile inatakiwa iende huko.

Bahati mbaya sana tayari imetangazwa kuwa hakutakuwa na VAR kwa sababu mbalimbali, kwani baadhi ya waamuzi ndiyo kwanza wapo kwenye mafunzo.

Kwa maana hiyo mpaka watakapomaliza kusoma, mzunguko wa pili tayari utakuwa umeshaanza, hivyo hakuna ulazima wala umuhimu wowote wa kutumia teknolojia hiyo, hivyo msimu ujao teknolojia hiyo inaweza kuanza kutumia.

Hata hivyo, nimemsikia Rais wa TFF, Wallace Karia, akisema moja ya changamoto ni kwamba viwanja vingi nchini havina miundombinu ya kufunga na kutumia VAR.

> **Hata hivyo, nimemsikia Rais wa TFF, Wallace Karia, akisema moja ya changamoto ni kwamba viwanja vingi nchini havina miundombinu ya kufunga na kutumia VAR.**

Ni kweli kabisa, kwa maana hiyo kama kweli msimu ujao Tanzania inataka kutumia VAR kwenye mechi zake za ligi kunatakiwa mjadala kwa wadau wa soka na watoke na msimamo wa pamoja.

Kwanza kabisa ieleweke kuwa ili ligi iwe bora na iwe ya haki ni lazima mechi zote zitakazochezwa zinapaswa ziwe na VAR.

Haiwezekani mechi inazocheza Simba, Yanga ziwe na VAR, halafu Pamba Jiji inacheza na KenGold hakuna teknolojia hiyo. Hiyo si haki na haileti ile maana ya mchezo wa soka 'fair play'. Kama nchi inataka kuwa na VAR, viwanja vyote nchini vifungwe teknolojia hiyo, kama haiwezekani basi ligi ichezwe tu bila kuwapo ili mradi tu kila mechi ichezeshwe sawa na nyingine. Ninaamini hakuna mechi bora kuliko nyingine kwenye ligi.

Timu zote zinataka ubingwa na zingine zinataka zibaki Ligi Kuu, na baadhi zinajinasua kushuka daraja, hizo zote zinahitaji maamuzi ya haki na ya uangalifu.

Ndiyo maana narudia kusema mjadala wa wadau wote wa soka nchini unatakiwa, kama kweli wanahitaji ligi yenye matabaka ya maamuzi yenye VAR, au yenye haki sawa kwa wote.

Mimi nadhani kwa hali hii, msimu ujao TFF na wadhamini wajitahidi kupata VAR Mobile nyingi ambazo zinaweza kumaliza tatizo hilo na si za kufunga. Kama bado viwanja vingi hapa nchini vina mapungufu au miundombinu yake ni hafifu kufunga mitambo hiyo, basi hakuna haja ya kuleta VAR ya kufunga, badala yake zile zinazohamishika ambazo zitakuwa zipo kwenye magari tu kama ile ambayo imeahidiwa na wadhamini.

Nadhani aina hizi za VAR ndizo zitakazofaa nchi yetu kutokana na aina ya viwanja vyetu mpaka hapo vitakapoboreshwa kuwa vya kisasa zaidi.

## HABARI KITAIFA



Makamu wa Rais Dk Philip Mpango akisalimiana na viongozi mbalimbali wa Arusha wakati alipowasili mkoani Arusha jana. Makamu wa Rais anatarajiwa kufungua Mkutano wa Mwaka wa Viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) utakaofanyika leo mkoani Arusha. **PICHA:MTANDAO**

# Hoja ya kada CCM yazua jambo

**Na Mussa Mwangoka,**
MPANDA

KAULI ya kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mbunge mstaafu wa Mpanda Mjini, Said Amour Alfi kwamba ni makosa makubwa kushabikia kukandamiza upinzani katika uchaguzi nchini, imezua jambo:

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Katavi, Teonas Kinyoto amedai kauli hiyo haiakisi uhalisia wa siasa zinazofanywa na chama hicho kikongwe nchini na anashangaa kutolewa na mwanasiasa huyo.

"Unajua siasa za CCM ni za kushindana kwa hoja na sera nzuri, ndizo zinazofanya ikubalike na kupata ushindi kwenye uchaguzi mbalimbali inaoshiriki. Shida ni kwamba hivi vyama vya upinzani havijipangi kikamilifu kushindana na CCM ambayo ina sera madhubuti," alidai.

Alitolea mfano Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27 mwaka huu, akieleza kuwa kuna vijiji 40 vyama vya upinzani havikusimamisha wagombea mkoani Katavi. Alitaja hali hiyo ni ishara kwamba "bado wanajitafuta".

Alisema hoja ya baadhi ya watendaji wa serikali waliosimamia uchaguzi kuruhusu kura feki kuingizwa katika masanduku na watu wasio na sifa kupiga kura, si za kweli kwa kuwa vyama vyote vya siasa viliweka mawakala wa kuangalia mchakato wa zoezi la upigaji kura na walitia saini fomu za kukubali matokeo.

Mwenezi huyo alipoulizwa kama kuna hatua zitachukuliwa dhidi ya mwanasiasa huyo kutokana na kauli yake hiyo, alisema chama kina taratibu zake, lakini kwa sasa hawezi kuzungumza lolote.

Wiki iliyopita, katika mazungumzo maalumu na waandishi wa habari nyumbani kwake mjini Mpanda, Alfi ambaye aliwahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa na kuhudumu ubunge wa Mpanda kwa zaidi ya miaka 10 kupitia CHADEMA kabla kurejea CCM, alisema:

"Sisi Chama Cha Mapinduzi tutafanya makosa makubwa sana kama tutatumia rasilimali zetu, nguvu zetu na maarifa yetu kuua upinzani! Lazima tuache upinzani ukue, una faida nyingi sana katika ustawi wa taifa hili."

Alitolea mfano kuwa wakati wa utawala wa awamu ya nne, mikoa ya Kanda ya Magharibi kwa maana ya Rukwa, Katavi, Tabora na Kigoma ilikuwa haijafunguka kimiundombinu, hivyo kutofikika kiurahisi. Nguvu ya vyama vya upinzani ilisaidia serikali kuifungua mikoa hiyo kimiundombinu.

Alisisitiza upinzani ni kichocheo cha maendeleo na ni fursa kwa serikali kukosolewa na hivyo kurekebisha upungufu uliopo na hatua stahiki zikachukuliwa.

Kada huyo wa CCM alisema serikali awamu ya tano ilijieleza "kuumaliza upinzanina ilifaulu kufanya hivyo", hali aliyoitaka imesababisha kutokuwapo watu au wanasiasa wanakosoa, kitu ambacho kwa mtazamo wake ni hatari kwa ustawi wa maendeleo ya taifa.

"Niwaeleze wana CCM wenzangu; tutakuwa tukijidanganya kama tutaamini kwamba tumeua upinzani. Kiuhalisia upinzani hauonekani ila umo katika mioyo ya watu... tusijidanyanye," alitoa tahadhari.

Aliweka wazi kuwa yeye binafsi hakufurahishwa na mchakato mzima wa uchaguzi huo, ikiwa pamoja na matokeo yake. Alidai watendaji wa serikali walifanya mambo ambayo anaamini hawakuagizwa na CCM bali kwa matakwa yao binafsi tu wakawakandamiza wapinzani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***

# Ulega ashtuka kusuasua miradi ya barabara Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega ametoa siku tatu kwa mkandarasi anayetekeleza mradi wa upanuzi wa barabara ya Ubungo - Kimara, kuongeza idadi ya wataalamu, vibarua na kufunga taa nyakati za usiku, ili kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

Pia amemwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Balozi Aisha Amour kuwasimamia makandarasi wanaotekeleza ujenzi wa miradi wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam, ili wafanye kazi usiku na mchana kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam alipozuru na kukagua mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu ateuliwe na Rais Samia Suluhu Hasan kuongoza wizara hiyo.

Akiwa katika ziara hiyo, Ulega aliagiza ujenzi wa miundombinu hiyo uende sambamba na uwekaji taa za barabarani kwa ajili ya ulinzi na usalama na kupendezesha mandhari ya jiji hilo.

Pamoja na mambo mengine, Ulega hakuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi wa BRT awamu ya kwanza inayoanzia Ubungo hadi Kimara ambao hadi sasa umefikia asilimia 26.

"Ni ukweli usiopingika kwamba kipande hiki cha kutoka Ubungo - Kimara ni kisumbufu mno, foleni ni kubwa sana, watu wanateseka na kupata adha, hivyo mkandarasi fanya kazi usiku na mchana, umechelewa sana na hatutaki kuona watu wanaatabika hapa," aliagiza.


Pia alisisitiza kutowavumilia makandarasi wazembe wanaoshindwa kutekeleza miradi kwa wakati na kuahidi kuwachukulia hatua za kimkataba na wengine kutopatiwa kazi nyingine za ujenzi nchini.

Vilevile, alisema hajaridhishwa na maendeleo ya ujenzi miundombinu ya BRT awamu ya tatu inayoanzia katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto unaotelelezwa na mkandarasi Sinohydro kwa Sh. bilioni 231 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika Machi mwakani.

Mbunge wa Ukonga na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, akiwa katika ziara hiyo, alisema ujenzi wa mradi wa BRT awamu ya tatu ukikamilika, utaongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi wa Ukonga na kupunguza muda wa usafiri kutoka saa mbili kwa magari ya kawaida hadi dakika 45 na kwa mabasi ya mwendo kasi dakika 30.

Msimamizi wa miradi ya ujenzi wa BRT kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Frank Mbilinyi alisema mradi wa BRT ulibuniwa mwaka 2004 chini ya Halmashauri ya Jiji kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***



CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30828 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

IBRAHIM M. MAHMOUD ........ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*


To: Ibrahim M. Mahmoud of Kisarawe II Area, Kigamboni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM



CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30825 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

RAJABU NASSORO ........ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Rajabu Nassoro of Kibada Area, Kigamboni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

# Mahakama ya Mafisadi yamwachia huru, jaji ashangazwa na upelelezi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imemwachia huru Lucy Ndunguru baada ya kumwona hana hatia katika shtaka la kusafirisha dawa za kulevya.

Hukumu hiyo imetolewa mbele ya Jaji Sedikia Kisanya baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili na kubaini upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha kosa bila kuacha shaka.

"Haijulikani upande wa mashtaka ulifanya haraka kumshtaki mshtakiwa au ilikuaje. Shauri linaonesha upungufu katika upelelezi, hali inayosababisha asiyekuwa na hatia anashikiliwa wakati aliyetenda kosa yuko huru hajakamatwa," alisema Jaji Kisanya. Akisoma hukumu, jaji huyo alisema mshtakiwa alikamatwa Agosti 14 mwaka 2023, maeneo ya Mlandizi, wilayani Kibaha akiwa na kilo 115 za dawa za kulevya aina ya bangi.

Jaji alisema mshtakiwa alikana mashtaka na upande wa Jamhuri uliita mashahidi sita na vielelezo saba. Mshtakiwa alijitetea mwenyewe na kuita shahidi mmoja.

Jaji Kisanya alisema katika utetezi wake, mshtakiwa alidai dawa za kulevya zilikutwa katika chumba cha kaka yake.

Alisema hoja kubwa ni kama ushahidi umethibitisha shtaka dhidi ya mshtakiwa bila kuacha shaka yoyote.

Ilidaiwa katika ushahidi kwamba Agosti 14, 2023, polisi walifanya upekuzi katika nyumba anamoishi mshtakiwa na kaka yake maeneo ya Mlandizi na kukamata magunia manne ya dawa za kulevya aina ya bangi katika chumba ambacho mshtakiwa anadai cha kaka yake .

"Jamhuri walipaswa kuleta ushahidi kuonesha mshtakiwa alihusika lakini katika ushahidi hata mpelelezi hakueleza chochote kuhusu chumba kilichokutwa na dawa za kulevya kama cha mshtakiwa.

"Ushahidi wa shahidi wa pili upande wa mashtaka unaungwa mkono na shahidi huru na shahidi wa pili wa upande wa utetezi ambao walidai mifuko minne ya dawa ilikutwa katika chumba ambacho mshtakiwa aliwaambia cha kaka yake," alisema Jaji Kisanya.

Alisema kujua umiliki wa chumba kilichokutwa na dawa za kulevya kulikuwa muhimu na hakuna ushahidi mwingine uliotolewa. "Sioni sababu za msingi za kutupilia mbali utetezi wa mshtakiwa aliotoa tangu mwanzo kwamba chumba anakimiliki kaka yake.

"Katika shauri hili ushahidi pekee uliomhusisha mshtakiwa na dawa za kulevya ni ushahidi wa shahidi wa pili ambaye alidai mshtakiwa alikuwa na funguo za chumba na alifungua chumba hicho. "Ushahidi huo unapingana na ushahidi wa mashahidi wengine waliodai chumba kilifungwa na kilifunguliwa kwa kuvunja kufuli, shahidi alitumia jembe kuvunja kufuli.

"Hata mpelelezi ambaye ni shahidi wa sita alidai mlango ulivunjwa, mkanganyiko huo wa mashahidi unaleta shaka kuhusiana na ushahidi wa shahidi wa pili," alisema.

Alisema kama mshtakiwa hakuwa na funguo za chumba, kuna uwezekano kaka yake anatumia chumba hicho na kuhifadhi dawa. Jaji Kisanya alisema kuna shaka ambayo ilitakiwa kuondolewa. Kulitakiwa kuwapo ushahidi wa kuonesha mshtakiwa alikuwa anajua kuwapo kwa dawa hizo za kulevya.

"Kesi dhidi ya mshtakiwa ni dhaifu, ushahidi haukuonesha alikuwa na ufahamu wa hizo dawa, haijulikani upande wa mashtaka walikuwa na haraka ya kumshtaki mshtakiwa au ilikuwaje.

"Jamhuri haikuthibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa, shauri linaonesha upungufu katika upelelezi. Hii inasababisha asiyekuwa na hatia anashikiliwa na aliyetenda kosa anakuwa huru. Hajakamatwa.

"Ni muhimu kupeleleza mashauri vizuri kuepuka haki kutotendeka, hasa haya mashauri ambayo hayana dhamana.

"Mahakama inamwachia huru Lucy. Hana hatia! Kielelezo cha dawa za kulevya ziteketezwe na wakati wa utekelezaji ukisubiriwa, kielelezo kiwe mikononi mwa polisi," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***

# Othman: Mifumo bora ya sheria, sera ni muhimu kwa uchumi wa soko huria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman kuwa ili kuingia katika uchumi wa soko huria, kunahitajika mifumo, sheria na sera zilizo bora katika nchi.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa mkutano wa nne wa taasisi ya Wakfu wa Maalim Seif Sharif uliofanyika Mji wa Zanzibar, akisisitiza kuwa kuweka mifumo, sheria na sera bora kutawavutia wenye mitaji, uzalishaji na uwezo wa kulitumia soko hilo huria.

Alisema jambo lingine muhimu linalohitajika ni uongozi bora ambao utakuwa na maono ya kutunga sera, sheria sahihi na kuweka miundombinu bora ya usimamizi wa sera na sheria za nchi.

Makamu wa Rais aliisema lazima kuwapo na utendaji wenye ufanisi kwa sababu bila ya hayo si rahisi kulitumia soko huria pamoja na teknolojia sahihi katika uzalishaji na udhibiti wa ubora inahitajika.

"Tunaweza katika nchi tukawa na kila kitu ikiwamo ardhi ya kutosha. Ninaamini Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza barani Afrika na pengine duniani kwa kuwa na ardhi ya nzuri ya uzalishaji, lakini kikwazo ni teknolojia sahihi ya kuzalisha," alisema Othman.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Muhammed Aboud alisema Maalim Seif alisimama na watu nchini na duniani katika kusimamamia haki, uadilifu, umoja na maendeleo.

Alisema mada zitakazowasilishwa ni muhimu kwa Zanzibar kwa sababu suala la demokrasia, uchumi na ajira ni muhimu katika nchi hasa katika wakati huu wa kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Alisema Zanzibar itafanikiwa iwapo wananchi wataimarisha umoja wao katika jambo ambalo ni msingi wa maendeleo na mafanikio ni umoja wa wazanzibari.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalndo, Nassor Ahmed Mazrui alisema demokrasia ina nafasi kubwa katika maendeleo ya kiuchumi, ambao dunia nzima ina taharuki katika kuona demokrasia ina nafasi kubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kuzalisha ajira.


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30832 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

RIZWAN ESMAIL MOHAMED ........ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Rizwan Ismael of Plot No. 981, Msasani Area, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIVUKONI/KINONDONI, DAR ES SALAAM

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM



CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: ........OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

ALEXANDER L. KIMARIO 30830 ........ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Alexander Kimario of Temboni Street, Kimara Area, Ubungo Municipality

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

182958



CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: ........OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

STRATON RICHARD MAKUNDI 30837 ........ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Straton Richard Makundi of Plot No. 47, Mikocheni Area, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

RESIDENT MAGISTRATE COURT KINONDONI, DAR ES SALAAM

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

## Jeshi la Polisi lapiga marufuku wanafunzi kupanda bodaboda

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha limewapiga marufuku madereva bodaboda kusafirisha wanafunzi pamoja na kuwataka wamiliki wa shule kuacha kusafirisha wanafunzi na walimu wa jinsia moja katika gari, badala yake kuwepo na jinsia tofauti.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Murieti, ASP Chate alitoa onyo hilo wakati wa hafla ya kuwapongeza wahitimu wa darasa la saba, awali na msingi waliofanya vizuri katika mitihani yao katika Shule ya Socrates.

ASP Chande alimwakilisha OCD Wilaya ya Arusha Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Georgina Matagi.

Alisema jukumu la jeshi hilo ni kuendelea kutoa elimu pamoja na kuwafundisha adabu wanaokiuka sheria.

"Ni marufuku bodaboda kusafirisha wanafunzi wa shule na tutambue tu usafiri huu siyo salama hasa unapobeba watoto wengi kwa wakati mmoja, unakuta bodaboda zinazungukia kila nyumba kukusanya watoto na kuwapeleka shuleni jambo ambalo hata wazazi wanaofanya hivyo hawajui thamani ya watoto wao" alisema na kuongeza:

Alitolea mfano wa kesi ya ubakaji iliyopelekwa katika kituo hicho na kulipofanyika uchunguzi ilibainika kuwa usafiri uliotumika, katika gari hilo la wanafunzi halikuwa na mwalimu wa kike,". alisema

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Murieti, Ngolo Matugolo alitoa rai kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto wao msimu huu wa likizo, sikukuu za mwisho wa mwaka na wasiruhusu wageni hasa watu wazima kulala na watoto wanapokuwa wametembelea nyumbani kwa ajili ya likizo.

"Nitoe wito kwa wazazi na walezi sote tunafahamu huu ni mwisho wa mwaka ni dhahiri kuwa tunatembelewa na ndugu jamaa na marafiki, niwaombe tu msimwamini mtu hata kuacha watoto walale nao chumba kimoja.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Joyce Msofe pamoja na mmoja wa wazazi wakizungumzia suala la ukatili katika jamii waliwataka wazazi na walezi kuacha kukumbatia watoto wao na kuwasahau wa wengine jambo ambalo limekuwa changamoto kuweza kurekebisha maadili katika Jamii.

Hata hivyo akieleza ugumu na mafanikio ya utekelezaji wa mtaala mpya, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Socrates, Wycliffe Rioba alieleza namna ambavyo walipata shida kutekeleza mtaala kutokana na mfumo waliozoea wanafunzi ambapo kwa sasa wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza mtaala huo.

Alisema Shule ya Awali Socrates huamini kufanya mahafali baada ya matokeo ya mitihani ya taifa ya darasa la saba kwa lengo la kuwapongeza wahitimu na kuwapa nasaha za kuanza hatua mpya ya elimu ya sekondari ambapo wahitimu nane walitunukiwa vyeti vya elimu ya msingi, huku zaidi ya wanafunzi 70 wa awali wakitunukiwa vyeti vya kuingia darasa la kwanza.

# Jela miaka 30 kwa kumwingilia kinyume cha maumbile mwanamume mwenzake

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, imemhukumu mkazi wa Majengo Sanya Juu, Wilson Mollel (29), kwenda jela miaka 30 kwa kosa la kumuingilia kinyume na maumbile, mwanaume mmoja (jina limehifadhiwa) (45), ambaye walikuwa wakiishi wote.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Elibahati Petro.

Mwendesha Mashitaka wa Serikali, Kurwa Mungo, alidai kuwa tukio hilo lilitokea Januari mwaka huu katika eneo la Majengo, majira ya jioni.

Kesi hiyo ilikuwa na mashahidi sita akiwamo mwathirika, daktari pamoja na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sanya Juu.

Kurwa alidai kuwa siku ya tukio, mshitakiwa waliondoka na rafiki yake na kwenda kupata kinywaji cha pombe katika moja ya baa iliyopo eneo hilo.

Alidai walikunywa na kulewa, kwamba mshitakiwa baada ya kuona rafiki yake amelewa alimchukua na kurudi naye wanapoishi.

**Kurwa alidai kuwa siku ya tukio, mshitakiwa waliondoka na rafiki yake na kwenda kupata kinywaji cha pombe katika moja ya baa iliyopo eneo hilo.**

Kurwa alidai baada ya hapo mshitakiwa alifunga mlango na kuanza kumlawiti mwenzake, baada ya kufanya kitendo hicho na pombe ilipoisha kichwani alikuta amefanyiwa kitendo hicho na kuamua kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria.

Kurwa alisema kitendo hicho ni kinyume Kifungo cha 154 (1) (a) cha Kanuni ya Adhabu 16 iliyofanyiwa marejeo 2022, na kwamba kesi hiyo ya namba 1414/2024.

Wakati wa kutoa hukumu hiyo Hakimu Elibahati alisema ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hizo alimuhukumu kwenda jela miaka 30.



Baadhi ya wafanyabiashara ya madini wakibadilishana mawazo kwenye mnada wa madini ya vito ulioandaliwa na Wizara ya Madini ambapo gramu 184.06 za thamani ya Sh.bilioni 3.1 ziliuzwa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wahitimu chuo kikuu tumieni utafiti kutatua changamoto

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Chande amewataka wanafunzi waliohitimu katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), kutumia matokeo ya utafiti waliofanya kutatua changamoto zinazoikabili jamii badala ya kuzifungia kabatini.

Alisema hayo juzi jijini Arusha alipomwakilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba wakati wa mahafali ya 26 IAA.

"Katika kukamilisha safari yenu ya masomo baadhi yenu mmefanya utafiti na wengine tasnifu zenu zimechapishwa kwenye machapisho mbalimbali ndani na nje ya nchi kama takwa la chuo kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya kuhitimu ngazi husika," alisema.

Aliongeza: "Tumieni matokeo ya utafiti wenu kuisaidia jamii kukabiliana na changamoto kwenye maeneo mliyobaini endapo mtabaki na matokeo ya utafiti huo mtakuwa hamjawasaidia Watanzania".

Licha ya kuagiza kuwa tafiti hizo zisiishie kwenye kabati, maktaba na kwenye machapisho baada ya kuhitimu, amewataka wahusika kushirikiana na jamii kuhusiana na matokeo ya utafiti huo ili zitumike kuleta mabadiliko chanya na kuongeza tija kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii.

Pia, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh.bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati wa miundombinu ya elimu, kuwaendeleza walimu kielimu, kuanzisha mitaala mipya na kuhuisha iliyoko ili iendane na mahitaji ya jamii na soko la ajira.

Aidha, alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), imetoa Sh.bilioni 40 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu chuoni hapo.

Mkuu wa Chuo cha IAA, Prof.Eliamani Sedoyeka, alisema wahitimu 5,854 wamehitimu na kati yao wanaume ni 3,601 na wanawake ni 2,253 ambao wametunukiwa astashahada, stashahada, shahada na shahada za uzamili katika fani mbalimbali.

Alisema wataendelea kufanya utafiti mbalimbali kwa lengo kufahamu mahitaji halisi ya Watanzania na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa mtu mmoja mmoja, taasisi na mashirika katika sekta ya Umma na binafsi.

Aidha alisema kwenye mahafali hayo, IAA kwa mara ya kwanza wamefanikiwa kutoa wahitimu wa kwanza katika kozi tatu ambazo ni shahada ya usalama wa mtandao, shahada ya uanagenzi katika usimamizi wa utalii na ukarimu na shahada katika menejimenti ya maktaba na taarifa.

Vilevile, alisema dhamira ya chuo hicho ni kuendelea kuanzisha mitaala inayokidhi mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi IAA, Dk. Mwamini Tulli, aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Fedha, taasisi, mashirika na wadau mbalimbali kwa michango yao ambayo imekiwezesha chuo hicho kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na ushauri.





# Waziri: Ucheleweshaji kesi za ardhi pasua kichwa

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini amesema ucheleweshaji wa kesi za migogoro ya ardhi bado ni tatizo nchini kutokana na kuchukua muda mrefu wa kuanzia miaka minne na zaidi bila kutolewa maamuzi.

Kutokana na hali hiyo, Sagini amebainisha mpango wa serikali kupitia wizara hiyo kuhakikisha wanapunguza muda wa uendeshaji wa mashauri hayo ili kutoa nafasi kwa watu kupata haki zao kwa wakati na kuendelea na mambo mengine.

Sagini alibainisha hayo juzi wakati akizindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria 'Mama Samia Legal Aid Campaign' iliyofanyika katika Manispaa ya Musoma mkoani Mara.

“Sasa kama mashauri ya ardhi yanaenda miaka mitatu, mpaka minne au zaidi tofauti na mashauri ya jinai yenyewe yanakamilika kwa miezi sita, kuna haja ya kuharakisha na tumepata waziri mpya tutamshirikisha hili na mwenzie wa ardhi ili jambo lifanyiwe maamuzi haraka,” alisema Sagini. Kuhusu taratibu za mirathi, Sagini alisema hakuna ubaguzi kati ya mwanamke na mwanamume katika kumiliki mali na kuwa watoto wana haki hiyo pia, kwa mujibu wa utaratibu unaowekwa na mahakama.

“Msimamizi hapaswi kufikiri yeye ndiye mmiliki wa mali, ndiyo maana tumeleta msaada wa kisheria jamii ielewe mambo haya,” alisema Sagini.

**“Msimamizi hapaswi kufikiri yeye ndiye mmiliki wa mali, ndiyo maana tumeleta msaada wa kisheria jamii ielewe mambo haya,” alisema Sagini.**

Alisema kampeni hiyo inalenga kuongeza uelewa wa masuala ya sheria kwa jamii hususani haki za wanawake, watoto, sambamba na hilo kuimarisha huduma ya ushauri wa kisheria kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Awali Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mara, Alphan Haule, alisema kutokuwepo kwa baraza la ardhi wilayani Rorya pamoja na sintofahamu ya umiliki wa mali za marehemu eneo la mirathi kati ya ukoo au watoto na wajane limekuwa tatizo katika maeneo hayo na kuwa kutokana na ufafanuzi uliotolewa wanatarajia kulimaliza.

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala Katiba na Sheria, Boniphace Nyangindu alisema kampeni hiyo inafanyika nchi nzima ambapo tayari imefanyika katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida, Njombe, Iringa, Songwe na sasa Mara.

“Mpaka sasa zaidi ya wananchi laki laki nne wamepata huduma. Hii ni jitihada kubwa inayofanywa na serikali, pamoja na majukumu mengine ya bunge, huduma hii ni sehemu ya wajibu wetu kwa umma wa Watanzania” alisema.

Kauli mbiu ya kampeni hiyo ni msaada wa kisheria kwa haki, usawa, amani na maendeleo ililenga kutetea haki za wananchi wanyonge na kupinga vitendo vya uvunjifu wa haki ambako kwa Mara inatarajiwa kumalizika Desemba, 20 mwaka huu.



Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani Makao Makuu (ACP), Michael Stephen, akitoa elimu ya kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa Maofisa usafirishaji Manispaa ya Shinyanga ili kudhibiti ajali hasa kuelekea mwisho wa mwaka. **PICHA:MARCO MADUHU.**

# Bodaboda waonywa uvunjaji sheria mwisho wa mwaka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani Nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ASP), Michael Stephen amewaonya madereva wa pikipiki juu ya ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani kuelekea mwishoni mwa mwaka.

ASP Stephen alibainisha hayo juzi wakati akitoa elimu ya kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa bodaboda mkoani Shinyanga, iliyolenga kudhibiti ajali ambazo zimekuwa zikitokea kuelekea mwisho wa mwaka na mwaka mpya.

Alisema Jeshi la Polisi linatambua umuhimu wa bodaboda na elimu wanazowapatia mara kwa mara zinalenga kuwakumbusha juu ya kutii na kuzingatia sheria za usalama barabarani kudhibiti ajali zisizo za lazima zitokanazo na uzembe wa dereva.

Alitaja mambo ambayo madereva hao wanapaswa kuzingatia kuwa ni pamoja na kuvaa kofia ngumu, kutoendesha mwendokasi, kutozidisha abiria, kuchukua tahadhari wakati wa kupishana barabarani, kuvaa sare, kuwa na leseni pamoja na vyombo vyao kuvikatia bima.

Kaimu Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga, SP Methew Ntakije, alisema bodaboda wamekuwa na utaratibu wa kuweka kofia ngumu chini ya miguu badala ya kuzivaa kichwani na kueleza kuwa watakaoendelea kufanya hivyo watachukuliwa hatua za kisheria.

Mkuu wa Polisi Jamii Mkoa wa Shinyanga (ACP), Fraterine Tesha, aliwataka bodaboda hao kushirikiana kikamilifu na polisi kata kuripoti vitendo vya uhalifu na wahalifu kwani wanakuwa nao mitaani.

# ‘Drones’ kutumika kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MKURUGENZI wa Uvuvi nchini, Prof. Mohamed Sheikh amesema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanatarajia kuanza kufanya doria kwa kutumia ndege zisizo na rubani ili kuweka usalama wa viumbe katika maji.

Prof. Mohammed alibainisha hayo jijini Mwanza, katika mkutano wa kupokea maoni ya kuboresha kanuni za uvuvi pamoja na wadau wa sekta hiyo.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha uchumi wa bluu utakaokuwa na tija kwa mwananchi na taifa kwa ujumla, hivyo itahakikisha inadhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na wadau.

“Tunaanzia na ndege tano na kwa Ziwa Victoria tutakuwa nazo mbili na hili zoezi litaanza mwaka ujao wa fedha, hatua hii itasaidia kutokomeza uvuvi haramu na kuwa na uhakika wa usalama wa viumbe maji,” alisema Prof. Mohamed

Aidha alisema sekta hiyo bado inachangia asilimia 1.8 katika pato la taifa kiwango ambacho ni kidogo kulinganisha na ukubwa wa uchumi utokanao na sekta hiyo, hivyo kutaja mkakati uliopo sasa kuwa ni kuhakikisha maboresho yenye tija yanafanyika.

Alisema maboresho hayo yanalenga kuvutia zaidi wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, hasa baada ya kuwa na uhakika wa mazingira mazuri na wingi wa rasilimali zilizopo.

“Tumekuwa na utaratibu wa kuyafunga maziwa kwa muda hasa katika shughuli za uvuvi wa dagaa, tumeona namna zoezi hili lilivyokuwa na tija wanaporudi kuvua upatikanaji unakuwa wa kiwango kikubwa na soko linakuwa zuri,” alisema Prof. Mohammed.

Wakati huohuo, imeelezwa kuwa kupanda kwa bei ya samaki katika mikoa ya Kanda ya Ziwa imezidi kushamiri, huku uvuvi haramu ukitajwa kuwa sababu kutokana na kuvuliwa kwa samaki wasiokuwa na sifa.

Samaki ambaye alikuwa akinunuliwa kwa Sh.3,000 hadi Sh.5,000 kwa sasa anauzwa kati ya Sh.10,000 hadi 15,000.

Njia mbalimbali za kudhibiti uvuvi haramu ikiwemo doria za askari, kuchoma nyavu na kukamatwa kwa mitumbi na wavuvi haramu zimeanza kutumia kuanzia miaka ya nyuma bila mafanikio.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Utafiti wa Mazingira la ACCORD Tanzania, mwaka 2021 ulibainisha kuwa ifikapo mwaka 2048 kutakuwapo na upungufu mkubwa wa samaki katika Ziwa Victoria, kutokana na uzalishaji samaki nchini kushuka kwa asilimia zaidi ya 50, kutoka tani 400,000 hadi tani 200,000, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Aidha utafiti huo haukupishana zaidi na ule uliofanywa na Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) mwaka 2005, ukieleza kuwa miaka 40 iliyopita mpaka kufikia mwaka huo aina 200 za samaki katika ziwa hilo wametoweka, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa ni uvuvi haramu na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Nipashe
Spotika



RAHA NA UTAMU WA LIGI KUU BARA... UKURASA 14



SALAH

# WANASOKA 10 BORA WA AFRIKA TISHIO ULAYA

**LONDON,** England

MATAIFA ya Afrika yanaweza yasiwe vinara katika ngazi ya kimataifa, lakini kwa muda mrefu yametoa wanasoka matata na bora zaidi duniani.

Unahitaji tu kutupia jicho lako nyuma katika miongo miwili iliyopita kwenye Ligi Kuu England ili kuona mastaa wa Afrika waalivyotamba katika daraja la hadhi ya juu zaidi duniani, huku nyota kama Didier Drogba, Yaya Toure na Michael Essien wakiwa na watazamaji wengi mno.

**Hata hivyo, baadhi ya vipaji vi kubwa zaidi barani Afrika bado vinafanya biashara yao katika ngazi ya juu, huku kizazi kipya nacho kikiibuka kwa kasi.**

Hapa tunawaangalia wanasoka 10 bora kutoka Afrika wanaotamba kwa sasa Ulaya...

**10. Victor Boniface**

Victor Boniface alikuwa sehemu muhimu ya ushindi wa Bayer Leverkusen wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu wa 2023/24. Raia huyo wa Nigeria alifunga mabao ya kufurahisha mapema katika kampeni ya Die Werkself hao, ingawa majeraha yalipunguza ufanisi wake.

Mshambuliaji huyo wa kati amethibitisha kuwa ni mahiri sana kutoka Union Saint-Gilloise ya Ubelgiji na tayari anafanya vema kwenye kwa uwezo wake mkubwa. Boniface ni jinamizi la beki anapokuwa fiti.

**9. Edmond Tapsoba**

Kipaji kingine cha Afrika kinachotamba pale Bayer Leverkusen. Huyu ni mchezaji wa Kimataifa wa Burkina Faso, Edmond Tapsoba akipanga safu yao ya ulinzi kwenye upande mwingine wa uwanja. Wakiwa wameunda sehemu ya mabeki watatu wa kati chini ya Xabi Alonso, Tapsoba pia alikuwa muhimu katika ushindi wa kwanza wa Leverkusen wa Bundesliga.

Nguvu, mbio na stamini ya Tapsoba katika kukaba humfanya kuwa mtu mgumu kukabiliana naye.

**8. Mohammed Kudus**

West Ham United ilipambana na baadhi ya vigogo wa Ulaya kuinasa saini ya Mohammed Kudus mwaka 2023, huku fowadi huyo wa zamani wa Ajax akiwa amevutia macho ndani na Ulaya kutoka pale Amsterdam.

Kudus haraka amekuwa akipendwa na mashabiki wa West Ham kwa mchanganyiko wake wa umaridadi, nguvu na upigaji mpira safi, akifunga mabao 14 katika msimu wake wa kwanza pale London. Bado kuna mengi zaidi kutoka kwa raia huyo wa Ghana.

**7. Andre Onana**

Msimu wa kwanza wa Andre Onana pale Manchester United ulikuwa mgumu sana. Hata hivyo, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Cameroon alianza kuonesha thamani yake ya pauni milioni 47.2 ambayo 'Mashetani Wekundu' walilipa kwa Inter Milan.

Msimu wa 2024/25 umemshuhudia Onana akizidi kujiamini na ndiye mlinda mlango hodari zaidi Ulaya kutoka barani Afrika wakati wa kampeni ya sasa.

**6. Nicolas Jackson**

Nicolas Jackson ambaye alishutumiwa sana amebadilisha sifa yake msmimu wa 2024/25. Baada ya kuhusishwa na makosa mengi katika kampeni yake ya kwanza pale Chelsea, mshambuliaji huyo wa Senegal alifanya kazi kwa bidii kurekebisha makosa yake msimu wa majira ya joto na akarudi mchezaji tofauti.

**5. Serhou Guirassy**

Nafasi ya kwanza ya Serhou Guirassy katika soka la Ujerumani haikuwa maalum. Alifunga mara tisa katika mechi 45 akiwa na Koln kabla ya kurejea Ufaransa. Lakini Stuttgart ilimchukua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Guinea msimu wa 2023/24 na ilionesha nyongeza ya mabadiliko.

Guirassy alifunga mabao 30 katika michezo 30 wakati Stuttgart ilipomaliza kama washindi wa pili wa Bundesliga na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kumfanya mshambuliaji huyo wa kati kusajiliwa na Borussia Dortmund.

**4. Ademola Lookman**

Ademola Lookman ndiye mchezaji pekee kutoka bara la Afrika kuteuliwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or 2024. Hiyo ilitokana na ushujaa wake katika fainali ya Ligi ya Europa 2023/24, akiifungia Atalanta hat-trick ya kuvutia dhidi ya Leverkusen.

Kumaliza kwa heshima katika nafasi ya 14 kunaonesha hatua ambazo Mnigeria huyo amechukua tangu mara kadhaa bila mafanikio akiwa na klabu tofauti vya England.

**3. Achraf Hakimi**

Achraf Hakimi si tu beki mwenye kipaji zaidi kutoka bara la Afrika, ni miongoni mwa mabeki bora wa kulia katika soka duniani. Raia huyo wa Morocco, ambaye alikuwa akivutia macho katika mbio za taifa lake hadi nusu fainali ya Kombe la Dunia 2022, aling'ara huko Dortmund kabla ya kuhamia Inter mnamo 2020.

**2. Victor Osimhen**

Mwanasoka Bora wa Afrika wa 2023, Victor Osimhen alijitengenezea sifa ya kuwa mmoja wa washambuliaji wazuri zaidi duniani wakati alipokuwa na Napoli. Lakini mzozo wake na klabu hiyo umemfanya kupelekwa kwa mkopo Galatasaray kwa kampeni ya 2024/25.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria ameanza kwa kasi ya ufungaji mabao mjini Istanbul. Iwapo atapata hatua yake inayofuata, Osimhen anaweza kushindana vema na Erling muongo mmoja ujao.

**1. Mohamed Salah**

Hakuwezi kuwa na mjadala kuhusu kipaji kikubwa zaidi kutoka barani Afrika kwa sasa ambacho ni Mohamed Salah.

Akiwa mmoja wa washambuliaji hatari zaidi katika miaka nane iliyopita, mshindi huyo na Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Afrika ameweka kiwango katika Klabu ya Liverpool na kuonesha dalili chache za kupunguza kasi katika siku za usoni.

## ISIKUPITE

KATIKA hatua kama hii msimu uliopita, Arsenal ilikuwa na pointi 36, nafasi ya pili, huku msimu uliopita kabla ya huo wakiwa wamekaa kileleni kwa pointi 40. Hadi sasa wamepoteza michezo miwili pekee, idadi sawa na misimu hiyo miwili iliyopita, lakini sare zimewagharimu msimu huu kwani inazo sita. Baada ya kushindwa kuifunga Fulham Jumapili ya Desemba 8, Arsenal imetoka sare mfululizo kwenye mechi za ligi kwa mara ya kwanza tangu Aprili 2023, huku sare tasa dhidi ya Everton juzi ikiwa ni ya kwanza kwao bila goli nyumbani tangu Januari 2023 dhidi ya Newcastle.





Kikosi cha timu ya Hispania

# TIMU 10 ZA TAIFA ZENYE NGUVU DUNIANI 2024

**NYON,** Uswisi

MWAKA 2024 umekuwa wa kipekee kwa mchezo wa soka hasa katika jukwaa la kimataifa, lakini sasa akili yote inaelekezwa kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2026.

Maandalizi ya kufuzu kwa michuano hiyo - inayoandaliwa kwa ushirikiano wa nchi tatu Marekani, Canada na Mexico -yanaendelea katika mabara mengi kabla ya Kombe la Dunia kufanyika majira ya kiangazi.

Nani atafanikiwa kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho chenye hadhi kubwa zaidi bado haijajulikana, ingawa mabadiliko ya muundo sasa yanahakikisha timu 48 zinacheza mashindano hayo.

Macho yataelekezwa kwa mataifa mashuhuri duniani katika mchakato wa kufuzu.

90min hapa inakuchambulia timu 10 za taifa zenye nguvu zaidi katika soka la kimataifa kwa sasa...

**10. Uruguay**

Mataifa sita ya COMEBOL (Shirikisho la Soka la Amerika Kusini), yanafuzu Kombe la Dunia la 2026 na washindi wa kwanza wa michuano hiyo, Uruguay wapo katika nafasi nzuri ya kupata nafasi yao.

'La Celeste' hao walikuwa katika kiwango cha kuvutia wakati wa michuano ya Copa America majira ya kiangazi na kufika nusu fainali kabla ya kutolewa na Colombia. Kikosi hicho cha kocha Marcelo Bielsa kilistahimili hali mbaya baada ya mchuano huo, lakini wakapata pointi nne katika mechi dhidi ya Colombia na Brazil katika kipindi cha mapumziko ya Kimataifa cha Novemba cha kufuzu kwa Kombe la Dunia.

Kulipiza kisasi kwa Colombia kulikuja kwa njia ya ushindi wa mabao 3-2, huku bao la Federico Valverde likiipa sare ya bao 1-1 na Brazil na kuwaacha Uruguay wakiwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa kufuzu kwa CONMEBOL.

**9. Italia**

Si siri kuwa Italia ilivumilia kampeni mbaya ya Euro 2024, lakini kocha wa zamani wa Napoli aliyeshinda Scudetto, Luciano Spalletti, amewasaidia Azzurri hao kupiga hatua tangu wakati huo.

Italia haikufungwa katika msimu wa 2024/25 wa kampeni ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mataifa ya UEFA hadi walipopoteza Novemba 20 kwa Ufaransa, na kukosa nafasi ya kwanza katika Kundi la 2 la Ligi A.

Baada ya kuzishinda Ufaransa, Ubelgiji na Israel, Italia itaivaa Ujerumani katika robo fainali ya Ligi ya Mataifa ya UEFA Machi mwakani.

**8. Brazil**

Baada ya kampeni mbaya ya Copa America msimu wa majira ya joto, Brazil wanajikuta katika hali nzuri tangu kurejea kwao kwenye mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la CONMEBOL.

Vinicius Junior na wenzake walishindwa kupata ushindi ugenini dhidi ya Venezuela kabla ya kuambulia sare ya nyumbani na Uruguay katika mapumziko ya kimataifa ya Novemba, na kuwaacha wakiwa nafasi ya tano kwenye kufuzu na pointi saba nyuma ya wapinzani wao Argentina waliopo kileleni.

Dorival Junior bado hajaonesha kuwa kwenye nafasi nzuri kama kocha mkuu wa nchi hiyo.

**7. Colombia**

Kupoteza kwa Uruguay na Ecuador kumepunguza kidogo hali ya kujiamini kwa Colombia, lakini kikosi cha Nestor Lorenzo kilibaki katika nafasi nzuri licha ya kushindwa Novemba.

Wakiwa wamechapwa na Argentina katika fainali ya Copa America 2024, Colombia waliwachapa mabingwa hao wa dunia katika mechi ya kufuzu ya Septemba, na wakaendelea kwa kuwafunga Chile mabao 4-0 Oktoba, mwaka huu.

Huku mchezaji wa Liverpool, Luis Diaz, akiwa katika kiwango cha hali ya juu na nyota wa zamani wa Real Madrid, James Rodriguez akiwa 'amefufuka', Colombia inapaswa kurahisisha njia yao ya kufuzu kwa Kombe la Dunia.

**6. Ureno**

Ureno walishindwa katika michuano ya Euro 2024 chini ya Roberto Martinez, lakini wamepoteza mechi nne pekee kati ya 26 zilizopita katika michuano yote huku kikosi chenye nyota wengi kikikua vizuri pamoja.

Cristiano Ronaldo alifunga mara kwa mara wakati Ureno wakijiweka sawa kupitia kundi lao la Ligi ya Mataifa ya UEFA, kwa kuzishinda Poland, Croatia na Scotland na kujihakikishia nafasi ya kwanza. Watacheza na Denmark katika hatua ya robo fainali.

Wakati Ureno ikijiandaa kuachana na Ronaldo katika miaka michache ijayo, mkongwe huyo amewanyamazisha wakosoaji wake wa Euro 2024 kwa kufunga zaidi katika mashindano ya Mataifa ya UEFA.

**5. Ujerumani**

Mchuano wa nyumbani uliahidi furaha kwa mashabiki wa Ujerumani baada ya siku kadhaa za giza chini ya kocha wa sasa wa Barcelona, Hansi Flick, lakini Euro 2024 ilikuja mapema sana kwa Julian Nagelsmann mwanzoni mwa mradi wake.

Ujerumani ilicheza vema msimu wa kiangazi na vipaji vyao vya vijana viling'ara, hata kama kuondolewa kwenye robo fainali mikononi mwa walioibuka kuwa mabingwa, Hispania, kulionekana kama nafasi iliyopotea.

Hata hivyo, Ujerumani haijashindwa tangu iliporahisishwa hadi kileleni katika kundi lao la Ligi ya Mataifa ya UEFA, ikishinda mabao 7-0 dhidi ya Bosnia na Herzegovina mnamo Novemba na ikionesha uwezo wa kushambulia chini ya Nagelsmann.

**4. England**

Huenda England haikushawishika kabisa wakati wa kupandishwa kwao Ligi A kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA, lakini hatupaswi kusahau kwamba, 'Simba Watatu' hao walitinga fainali ya Ulaya msimu wa majira ya joto.

Kocha Gareth Southgate ameondoka tangu wakati huo, na kuashiria alfajiri mpya kwa timu ya taifa huku Thomas Tuchel akijiandaa kuchukua jukumu la mechi yake ya kwanza Machi mwakani. Jambo kubwa kwao kwa sasa ni kushinda Kombe la Dunia 2026.

England ilionesha mwanga wa uwezo wao wa kushambulia chini ya kocha wa muda, Lee Carsley, lakini soka la kufikiria mbele na maendeleo ya vijana huenda yakakuzwa kwa mpangilio na uelekevu kutokana na kuteuliwa kwa kocha wa zamani wa Chelsea na Bayern Munich, Tuchel.

**3. Ufaransa**

Ufaransa ilitajwa kuwa bora kwa kuelekea Euro 2024, lakini iliishia nusu fainali. Kylian Mbappe hakuwa na kiwango cha kuvutia nchini Ujerumani na wachezaji wenzake hawakujiinua sana kwenye mashindano hayo.

Didier Deschamps alidumisha nafasi yake kama kocha mkuu kabla ya kufuzu kwa hatua ya makundi ya Ligi ya Mataifa ya UEFA na licha ya kuanza kwa kusuasua, 'Les Bleus' walijivuta hadi nafasi ya kwanza.

Kikosi chenye vipaji vya hali ya juu hurahisisha maisha kwa Deschamps, ambaye timu yake inabakia nafasi ya pili katika viwango vya ubora vya FIFA.

**2. Hispania**

Hispania ipo katika hali ya kuvutia zaidi. Tangu Kombe la Dunia la 2022, wamepoteza mechi nne pekee kati ya 27, na kutwaa ubingwa wa Euro 2024 chini ya Luis de la Fuente.

Kiwango chao chanya kimeendelea katika Ligi ya Mataifa ya UEFA, huku wakilenga kutetea taji lao. Ushindi mara tano na sare kutoka mechi sita za hatua ya makundi ilikuwa rekodi kali kwao Ulaya.

Wachezaji kama Lamine Yamal na Nico Williams wana matumaini ya kizazi kikubwa na La Roja watakuwa na nia ya kuendeleza kiwango chao cha kipekee katika Kombe la Dunia la 2026.

**1. Argentina**

Kunaweza kuwa na shaka kidogo juu ya timu bora ya kimataifa ulimwenguni jinsi mambo yanavyosimama. Mabingwa hawa wa dunia na washindi wa Copa America 2024, wameshinda michuano mitatu mikuu iliyopita waliyoshiriki, huku kocha Lionel Scaloni akiwa kwenye mhimili wa mafanikio yao ya kuvutia.

Lionel Messi anaendelea kuwa kiongozi kwa timu hiyo, Lautaro Martinez amekuwa mfungaji wao bora kwa sasa katika kila mechi za kimataifa.

Walikuwa bora zaidi msimu wa majira ya joto waliposhinda Copa America na wanaongoza katika kufuzu Kombe la Dunia kutoka Ukanda wa CONMEBOL, kwa sasa wamekaa pointi tano mbele ya Uruguay iliyo nafasi ya pili.

## Nukuu


"Nimesikitishwa kutoshinda mchezo, kuna timu moja tu ambayo inastahili kushinda nayo ni Arsenal. Tulitengeneza nafasi, lakini unapaswa [kufunga] kwa umiliki wote. Siwezi kuuliza zaidi kutoka kwa wavulana mbali na kuweka mpira wavuni. Tunapaswa kuwaweka kando," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta baada ya kulazimishwa sare tasa nyumbani juzi dhidi ya Everton**



"Baki kuwa mtulivu - ni rahisi kusema kuliko kufanya. Kurejea vizuri, ni chanya sana. Inasikitisha kuwa na watu 10 lakini tulionesha kupambana, " **Nahodha wa Liverpool Virgil van Dijk, baada timu yao kucheza pungufu kwa dakika 89 (pamoja na zile za nyongeza) dhidi ya Fulham na kutoka sare ya mabao 2-2 juzi.**



"Tutaona kama anaweza kucheza bila kuchukua hatari yoyote (ya kuumia), atasafiri kwa sababu tunadhani anaweza kupona jeraha hilo," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, akimzungumzia Kylian Mbappe, kuelekea mechi ya fainali ya Kombe la Mabara dhidi ya Al Ahly ya Misiri itakayopigwa Qatar keshokutwa, Jumatano.**



# RAHA NA UTAMU WA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imeingia raundi ya 14, huku baadhi ya timu zikiwa zimebakisha mechi moja kabla hazijamaliza mzunguko wa kwanza.

Mpaka kufikia sasa ligi hiyo msimu huu imekuwa na msisimko mkubwa, timu nyingi zimeonekana kujidhatiti na kutoa ushindani mkubwa.

Hali hiyo imesababisha hata ushindani kule juu ambao siku zote ulikuwa ni kwa Simba, Yanga na Azam FC, kuongezeka nyingine msimu huu kama Singida Black Stars na Tabora United ambazo zimeleta chachu kubwa katika vita ya kuwania ubingwa.

Hata timu zilizo kati nazo zimejitahidi sana kuhakikisha zinatoa upinzani mkali tofauti na msimu uliopita, ndiyo maana hadi kufikia leo hii hakuna timu yoyote iliyopoteza mechi kwa idadi ya mabao matano kama ilivyokuwa msimu uliopita ambapo mwanzoni mwa ligi tu, timu zilikuwa zikipigwa idadi hiyo ya mabao.

Inawezekana kabisa mzunguko wa pili ukawa mgumu zaidi kwani sasa kila timu itakuwa makini zaidi, kwa zile zinazotaka kutwaa ubingwa, kusalia Ligi Kuu, na zitakazojipapatua kujiondoa kwenye eneo la kucheza 'play off' na za kuepuka kushuka daraja.

Kumekuwa na matokeo ya kushangaza, ambayo hayakutarajiwa na mashabiki wengi wa soka, pia kuna matukio ambayo yameifanya ligi hiyo kuendelea kuvutia.

**1# Mechi moja penalti mbili**

Si mara nyingi sana kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara mwamuzi kutoa penalti mbili kwenye mchezo mmoja, lakini mpaka kufikia sasa, michezo miwili imetoa mikwaju minne ya penalti.

Agosti 25, mwaka huu, Namungo iliyokuwa nyumbani, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, ikicheza dhidi ya Tabora United, ilifungwa mabao 2-1, katika mchezo ambao ulizaa penalti mbili, moja kwa kila upande.

Djuma Shaaban alifunga kwa upande wa Namungo na Heritier Makambo alipachika bao kwa upande wa Tabora United.

Oktoba 25, mechi ya Ligi Kuu kati ya Azam FC dhidi ya KenGold iliyochezwa, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, pia ilizaa penalti mbili na zote ziliwekwa wavuni.

Katika mchezo huo ambao Azam ilishinda mabao 4-1, Azam ilipata penalti iliyowekwa wavuni na Feisal Salum 'Fei Toto', Kengold nayo ikapata yake, Joshua Ibrahim akaikwamisha wavuni.



Straika wa Simba, Steven Mukwala, akiwa kwenye staili yake anayoipenda kushangilia kila anapofunga bao.

**2# Mechi moja, mabao mawili ya kujifunga**

Moja kati ya matukio yaliyowaacha hoi mashabiki wa soka, ni mchezo mmoja kuwa na matukio mawili ya wachezaji kujifunga wenyewe, kitu ambacho mara nyingi ni nadra sana kutokea.

Ilikuwa ni Desemba Mosi kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Azam ilipokuwa mgeni wa Dodoma Jiji.

Katika mchezo huo ambao Azam ilishinda mabao 3-1, beki wa timu hiyo, Yannick Bangala, alijifunga kwenye dakika ya saba akiwa katika harakati za kuokoa, likiwa ni bao la kwanza la Dodoma Jiji, kabla ya Dickson Mhilu naye kuupachika mpira wavuni langoni mwao, akiwa katika harakati za kuokoa.

Hiyo ilikuwa ni dakika ya 59 na lilikuwa bao la tatu la Azam katika mchezo huo.

**3# Bao la kichwa nje ya boksi**

Katika mechi za Ligi Kuu mpaka sasa msimu huu kuna bao la kichwa lililofungwa nje ya boksi kitu ambacho si ni nadra kutokea hata ligi za Ulaya.

Straika, Ismail Mgunda wa Mashujaa FC, ndiye mchezaji pekee aliyefunga bao kwa kichwa akiwa nje ya eneo la mita 18 (nje ya boksi) la timu pinzani.

Bao hilo alilifunga, Oktoba 21, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika wakati timu yake ikicheza dhidi ya KenGold na kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Ilikuwa ni kama pasi ya juu iliyopigwa na Nyenyezi Juma, Mgunda aliruka juu na mabeki wawili wa KenGold kwa lengo la kutaka kuumiliki, lakini baada ya kuona wamemzidi maarifa, akaamua kuupiga kichwa ili uende langoni kwao.

Kwa bahati mbaya sana, kipa wa KenGold naye alikuwa ametoka langoni kutaka kusogelea eneo la tukio, akapishana na mpira uliokwenda moja kwa moja hadi wavuni.

Zaidi ya mabao 30 ya vichwa yaliyofungwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu msimu huu, ni hilo moja tu lililofungwa nje ya boksi.

**4# Bao la usiku zaidi Ligi Kuu Bara**

Moja ya matokeo ya kukumbukwa kwenye Ligi Kuu ni mechi iliyochezwa, Novemba Mosi, mwaka huu, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, Simba ikishinda bao 1-0 dhidi ya Mashujaa, ambalo lilifungwa kwenye dakika ya saba ya nyongeza.

Ni bao lililokuwa likisubiriwa kwa hamu na mashabiki wa Simba ambao mpaka wakati huo wengi walikuwa wameshakata tamaa na kuondoka uwanjani.

Kona iliyopigwa dakika za majeruhi na Awesu Awesu ilimkuta Steven Mukwala akiwa ameruka juu zaidi ya mabeki wote wa Mashujaa na kuujaza mpira huo wavuni, akiwafanya wanachama na mashabiki wa Simba wakipagawa kwa furaha.

**5# Yanga kufungwa na Tabora United**

Moja ya matokeo ya kushangaza kwenye Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 14, ni Yanga kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Novemba 7, mwaka huu.

Pamoja na kwamba ilitoka kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam, Novemba 2, mwaka huu, kwenye uwanja huo huo, lakini haikuamika kama Yanga ingekwenda kupoteza mechi ya pili mfululizo.

Si mara nyingi timu kubwa kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara. Na pia si mara nyingi kwa timu zinaoitwa au kujiita kongwe kama Simba na Yanga, kupoteza mechi kwa idadi kubwa ya mabao kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

**JE, WAJUA?**



LIVERPOOL juzi ilicheza pungufu kwa dakika 89 (ikiwa ni pamoja na zile za nyongeza), ikiwa na wachezaji 10 baada ya Andy Robertson kuoneshwa kadi nyekundu dakika ya 17 kwenye mechi dhidi ya Fulham na kutoka sare ya mabao 2-2. Hata hivyo ilionesha soka la kuvutia na kumiliki mchezo kwa asilimia 60, huku huu ukiwa mwanzo wao mzuri zaidi wa msimu tangu 2003.





# Mradi wa kilimo kunufaisha wakulima 5,400 mikoa mitatu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Kilimo kwa kushirikiana na Shiriki la Trees For The Future wameingia makubaliano ya kuendesha mradi wa kuviwezesha vyuo vya kilimo kutoa mafunzo ambayo yatawanufaisha wakulima 5,400 kutoka mikoa mitatu.

Mikoa hiyo ni Tabora, Singida na Mwanza kwa lengo la kuboresha maisha yao.

Mkurugenzi wa Shirika la Tree for the Future kwa Tanzania, Fredrick Mngube, akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo alisema utaanza kutekelezwa Januari mwakani katika mikoa husika.

"Mradi huu katika Mkoa wa Tabora utatekelezwa kwenye Wilaya za Uyui na Urambo, Mkoa wa Singida katika Wilaya ya Ikungu na Singida na katika Mkoa Mwanza utatekelezwa katika Wilaya za Magu na Misungwi," alisema.

Mngube alisema kitakachofanyika kwanza ni kuwafundisha wataalamu waliopo katika Chuo cha Tumbi kilichopo mkoani Tabora, Chuo cha Ukiruguru (Mwanza) na Chuo cha Mbondo kilichopo mkoani Kigoma.

Alisema baada ya kuwafundisha wataalamu hao na wao watakwenda kuwafundisha wataalamu wa ugani kuhusu bustani msitu ikoje na hao wataalam nao watakwenda kuwafundisha wakulima viongozi na kisha kuunda vikundi vya watu 30.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa mradi huo utafanya kazi katika kata tano kwa kila wilaya na hivyo kwa kila wilaya wanatarajia kuwa na wakulima 900 na hivyo kufanya jumla ya wakulima 5,400.

"Tunamshukru Rais Samia Suluhu kwa Hassan kwa kuwawezesha maofisa ugani vitendea kazi kama pikipiki, hivyo na sisi tutawasaidia wagani hao namna gani ya kuwasaidia wakulima kutatua changamoto zilizopo, " alisema

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Uendeshaji wa Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Idara ya Mafunzo ya Kilimo na Utafiti Wizara ya Kilimo, Godfrey Edward, alisema mradi huu utakuwa na mchango kwenye utekelezaji wa mipango mbalimbali ya wizara ambao ni mpango kabambe wa kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huu wizara imeandaa mpango mfupi wa agenda 10 ambazo lengo ni kuhakikisha kilimo kinakuwa kwa asilimia 10 ifikapo 2030.

"Ili kufikia malengo hayo lazima tija ya kilimo iongezeke na ili tija iweze kuongezeka inabidi wakulima watumie mbinu mbalimbali ambazo zinakabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Alisema matarajio ya wizara ni kuhakikisha mipango iliyowekwa kwenye utekelezaji wa mradi huo yanafikiwa na pande zote Shirika la Trees For Future na wizara ambapo kinachotakiwa ni ufuatiliaji wa karibu.

# Washauri kuongezwa makali sheria makosa ya ukatili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuangalia upya sheria inayotoa adhabu kwenye makosa ya ukatili ili kuiongezea makali yatakayosaidia kukomesha wimbi la matukio hayo kwa jamii.

Mkurugenzi wa Kituo cha Tanzania Shiriki Malezi Endelevu Kupinga Ukatili (TASHIMEKU) Dodoma, Makulu, Zawadi Mgeni alitoa rai hiyo jana kwenye maadhimisho ya tamasha la kupinga ukatili yaliyoandaliwa na kituo hicho jijini hapa.

Alisema sheria iliyopo kwa hivi sasa kutokana na kuongezeka kwa vitendo hivyo vya kikatili inaonekana bado haijakomesha vitendo hivyo kwa jamii.

"Nafikiri sheria ya adhabu iliyopo hivi sasa ni ndogo na ndiyo maana vitendo hivyo vya kikatili vimekuwa vikijitokeza kila siku, hivyo niiombe serikali iweke adhabu kali ambayo itakomesha tabia hiyo wanayofanyiwa watoto wa kike na wanawake kwa asilimia kubwa"alisema.

**Watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho, Lilian Said na Veis Hassan waliiomba serikali kuwachukulia hatua wamiliki wa vituo ambao wamekuwa wakivitumia...**

Watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho, Lilian Said na Veis Hassan waliiomba serikali kuwachukulia hatua wamiliki wa vituo ambao wamekuwa wakivitumia kama sehemu ya kujipatia fedha na mali zinazotolewa na wafadhili mbalimbali.

Walisema kuwa kuna baadhi ya wamiliki wa vituo wamekuwa wakiwatumia watoto hao kama sehemu ya daraja la kujipatia mali na fedha bila kujali kama misaada hiyo inatakiwa kufikishwa kwa walengwa ambao maisha yao ni duni.

Awali, Ofisa Ustawi wa Jamii Dodoma, Rachel Balisidya alisema wazazi na walezi wanapaswa kuongeza nguvu zaidi kwenye malezi ya watoto ili kuwaepusha na tamaa zinazoweza kuwasababishia kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Hivyo, aliwaasa mabinti wanaosoma kujilinda na kujiepusha na vishawishi vitakavyosababisha kuingia kwenye mitego itakayoua ndoto zao kielimu.



Mwenyekiti wa kijiji cha Buigiri wilaya ya Chamwino Festo Mwaluko alipokuwa akichangia mada kwenye warsha ya mafunzo elekezi kwa viongozi waliochaguliwa mwaka huu ngazi ya serikali za vijiji na vitongoji yaliyofanyika Buigiri. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanafunzi wa kike wapewa ujuzi matumizi TEHAMA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI wa kike kutoka shule mbalimbali za sekondari jijini Dodoma, wamenufaika na mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kutumia teknolojia hiyo.

Mafunzo hayo yaliyotolewa juzi kwa ushirikiano na wakufunzi kutoka Data Love Tanzania yanatarajia kuwafikia wanafunzi wa kike katika mikoa yote hapa nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kufunga mafunzo hayo, Joseph Sayi, alisema mpaka sasa mafunzo hayo yamewafikia wanafunzi 2,600 katika mikoa zaidi ya saba.

Alisema lengo lao ni kuona wanaifikia mikoa yote hapa nchini, dhamira yao ni kuwashawishi watoto wa kike kusoma masomo ya sayansi hususani ICT ambayo itawasaidia kutengeza mifumo mbali mbali kwa ajili ya kufanya shughuli za biashara pamoja na kurahisisha utendaji wao wa kazi.

"Mafunzo haya ni muhimu sana kaa wasichana kuanzia umri wa miaka 14 hadi 19, yanazidi kupanua wigo wa uwelewa wa maaomo ya ICT lakini pia kuwafanya wapende masomo ya Sayansi,"alisema Sayi.

Alisema katika mafunzo hayo walioita 'Code like a girl' wanafunzi hao wamejifunza vitu mbalimbali ikiwemo kutengeza website kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za biashara kupita mitandao.

Kutokana na hilo alisema mafunzo hayo yatazidi kutoa hamasa ya watoto wa kike kujifunza na kusoma masuala ya TEHAMA ili kupanua wigo wa kuja kujiajiri wao wenyewe hapo baadae.

"Huu ni mwanzo tu lengo letu ni kuona kila mwanafunzi wa kike anashiriki mafunzo ya ICT ambayo huwajengea uwezo wa kutumia teknolojia kubuni njia ya kutatua changamoto za kimaendeleo," alisema Sayi.

Mwanafunzi Natalia Mashaushi kutoka Shule ya Sekondari ya Kiwanja cha Ndege (Kndege), alisema programu hiyo imewasaidia kujua masuala mbalimbali ya TEHAMA ikiwamo matumizi yake.

Alisema wamefundishwa vitu mbalimbali vya teknolojia ikiwemo kubuni mifumo ambayo ikifanyiwa kazi inakwenda kuwa suluhisho la utatuzi wa changamoto mbalimbali kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mkufunzi na mratibu wa mafunzo hayo, Somoe Mkwachu alisema wanafunzi hao wameonyesha uelewa mkubwa katika mafunzo hayo ikiwamo kushindana kwenye ubunifu wa mifumo kupitia teknolojia.

Alisema wanafunzi hao kutoka shule tofauti baada ya mafunzo hayo kila mmoja alikuja na wazo ambalo walibuni teknolojia kwa ajili ya kulitatua ili kupata suluhisho.

Alisema: "Hi programu imewasaidia sana wanafunzi hawa kama unavyoona kila mmoja ametoka na ujuzi utakaomsaidia hapo baadae".





# Kiwanda kuzalisha mafuta ya parachichi kujengwa Njombe

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imesema imempata mwekezaji wa kiwanda cha kuzalisha mafuta ya parachichi ambacho kitawasaidia wakulima wa mkoa huo kuwa na soko la uhakika pamoja na kuwasaidia vijana kupata ajira.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wandishi wa habari baada ya kumaliza mazungumzo na viongozi wa Kampuni ya Avocado Avenue Tanzania LTD ambayo ndiyo inajenga kiwanda hicho.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho utasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kwamba zaidi ya ajira 300 zitapatikana kwa vijana wa mkoa huo pamoja na maeneo mengine nchini.

Alisema uwekezaji huo unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya kilimo katika mkoa huo hasa kilimo cha maparachichi.

Alisema kampuni hiyo imeonyesha dhamira ya dhati ya kushirikiana na serikali ya mkoa huo kuimarisha sekta hiyo na kuboresha maisha ya wakulima kwa kutoa ajira, elimu ya kilimo bora cha maparachichi na soko la uhakika la zao hilo.

**"Hili ndio lengo la Bodi ya Chai, Wizara ya Kilimo, na serikali kwa ujumla ni kuona tatizo la soko la chai nchini linafikia ukomo. Wakulima wasikate tamaa bodi ya chai ipo inaendelea kutafuta masoko...**

"Nawashukuru sana kwa kuja kuwekeza kwenye maparachichi mkoani kwetu, uamuzi wa kujenga kiwanda hapa Njombe utaongeza thamani ya matunda moja kwa moja kuanzia hapa na hii itakuza uchumi wa wakulima wetu na kuongeza ajira kwa wananchi hasa vijana," alisema Mtaka.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Avocado Avenue Tanzania Ltd, Amin Manji alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kutengeneza mafuta ya maparachichi ambayo ni muhimu kwa lishe na matumizi mengine.

Alisema kampuni hiyo ina mkakati ambao ni endelevu na hivyo wananchi watakuwa na uhakika wa soko la matunda yao na hivyo akawataka wakulima kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho.

"Tutakusanya maparachichi yote, yakiwemo yale yaliyokataliwa na wanunuzi wengine, tutazalisha mafuta na bidhaa zingine ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema Manji.

Alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kukamilika Machi mwaka 2025 ambapo kampuni hiyo itaanza kupokea matunda ya parachichi kutoka kwa wakulima mkoani humo.



Lori la mizigo lililobeba shehena ya mbolea likiwa limeacha njia na kutumbukia korongoni katika eneo la Malafyale kwenye mteremko wa mlima Iwambi jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Askofu awataka vijana kujiandaa na mabadiliko

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

VIJANA mkoani Njombe wametakiwa kujiandaa na mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani kwa kusoma na kujifunza vitu vipya pamoja na kutambua fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko katika maeneo yao ili kupunguza tatizo la ajira.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Njombe, Dk. George Fihavango aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya 13 ya Chuo cha Amani kilichopo mjini Njombe.

Alisema kwa kufanya hivyo itakuwa rahisi kuendesha maisha kutokana na fursa nyingi zilizopo na hivyo kinachotakiwa ni kukubali kubadilika kifikra na kuyapokea mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani.

"Mnaambiwa kutakuwa na tatizo la ajira lakini hatujaambiwa kama tutakuwa na tatizo la kazi, kazi zipo nyingi sana sasa umetoka na nyenzo gani za kukuwezesha kufanya kazi bila ya kuchagua lakini yenye staha na yenye kukupa kipato kwa sababu ukibadilisha fikra zako umejikomboa," alisema Askofu Fihavango.

Mkuu wa Chuo cha Amani, Fredy Ngimbudzi alisema wanatarajia kuongeza udahili wa wanachuo kutoka 136 waliopo sasa mpaka 250 ili kupanua wigo wa elimu na kukuza chuo.

"Matatizo yanayokabili chuo chetu ni kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi ukilinganisha na uwezo tulionao, hali hii inasababisha ugumu katika uendeshaji kufuatia makusanyo hafifu ya ada kutoka kwa wanachuo," alisema Ngimbudzi.

Mmoja wa wadau wa elimu mkoani Njombe, Eliud Nyauhenga aliwataka wahitimu wa chuo hicho kwenda kuzigeuza changamoto kuwa fursa uraiani, huku akiwataka kujiepusha na biashara haramu iliwemo ya dawa za kulevya.

"Vijana wengi wa kitanzania wamekuwa wakitumika vibaya kwa kusafirisha dawa za kulevya, kugeuza miili yao kuwa biashara ukiwemo ushoga kwa kisingizio cha ugumu wa maisha jambo ambalo linapaswa kupigwa vita kwa kutumia elimu mliyoipata," alisema.

Baadhi ya wahitimu wa chuo hicho akiwemo Sauda Wakara alisema watakwenda kutumia elimu walioipata kukabiliana na changamoto ya ajira ili kuepukana na magenge yanayoweza kuwaingiza kwenye matatizo.

# DC: Kampeni ya kisheria ya Samia itaondoa migogoro

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Herry James, amesema kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia itasaidia kuondoa migogoro iliyopo ya uelewa mdogo wa haki za binadamu.

Amesema pia itaondoa mila na desturi kandamizi, vitendo vya ukatili wa kijinsia, pamoja na imani za kishirikina zinazoawakabili wananchi wa mkoa huo.

James alisema hayo juzi alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba wakati akifungua mafunzo ya wajumbe wa kamati ya usalama ya elimu ya uraia na utawala bora inayoratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria.

Alisema Mkoa wa Iringia ni miongoni mwa mikoa iliyopata fursa ya kufikiwa na kampeni hiyo ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayofanyika kwa siku 10 katika mikoa minne.

Alisema inapaswa kutumika vizuri katika kutatua changamoto mbalimbali ambazo zimekuwapo kwa muda mrefu.

Serukamba alisema mafunzo kwa wajumbe hao yatawajengea uwezo viongozi katika ngazi mbalimbali za utawala, ili kuhakikisha wanazingatia misingi ya utawala bora, haki za binadamu, na demokrasia kwa vitendo.

Kadhalika alisema mafunzo hayo yanahusisha wajumbe wa Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya, baadhi ya wataalamu wa halmashauri, na watendaji wa kata zote za Mkoa wa Iringa.

"Kwa hiyo binafsi kwa mkoa wetu huu, kampeni hii pamoja na mafunzo vimekuja kwa wakati muafaka na tunaamini itakuwa ni msaada mkubwa kwetu kwenye shida ambazo zimetusumbua kwa muda mrefu, tuitumie kwa manufaa," alisema James.

Hivyo, alitoa wito kwa washiriki wa mafunzo hayo kushirikiana kutatua changamoto hizo kwa kushirikisha maarifa watakayopata, huku akiwataka viongozi na watendaji wa Mkoa wa Iringa kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha wananchi kutumia huduma za msaada wa kisheria.

Vilevile aliwahimiza washiriki kuhakikisha kuwa maarifa yatakayotolewa yanakuwa chachu ya mabadiliko katika utendaji wao wa kila siku.

Alisema: "Ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa elimu hii inasambazwa kuanzia ngazi ya familia hadi sehemu za kazi ili kujenga jamii yenye haki, amani, na utawala bora".



## Kairuki: Tanzania ni mshirika mahsusi Jukwaa la GEF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, Angellah Kairuki, amesema, Tanzania ni mshirika mahsusi na mwenye kujitolea kwenye juhudi za jukwaa la kizazi chenye usawa tangu lilipoanzishwa mwaka 2021.

Aliyasema hayo visiwani Zanzibar, katika ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo waratibu wa sekta binafsi katika Programu ya Kizazi chenye Usawa (GEF).

Alisema viongozi wakuu wa kitaifa wameonesha njia kwa namna ya kipekee katika uongozi wao ambapo Rais Samia Suluhu Hassan ni kinara kimataifa wa jukwaa hilo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kinara wa 'He For She'.

Alisema, katika maeneo ya kikazi ya jukwaa hilo kimataifa, Tanzania inajivunia kuongoza eneo la haki na usawa wa kiuchumi na inajipambanua kama moja ya mataifa machache yenye mpango kazi wa kitaifa na kamati ya kitaifa ya ushauri kuhusu jukwaa la kizazi chenye usawa.

Alisema pamoja na upekee wa Zanzibar, kiuchumi na kijamii, inayo fursa ya kipekee ya kuonisha vipaumbele vya Jukwaa la Usawa wa Kijinsia na ajenda ya maendeleo ya visiwa vyake.

Akifungua mafunzo hayo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema usawa wa kijinsia ni mojawapo ya nguzo muhimu katika kufikia maendeleo jumuishi na endelevu kiuchumi, kijamii, kisasa na kiutamaduni.

Alisema serikali kwa kuona umuhimu wa mafunzo hayo, imewashirikisha ili kuleta mageuzi chanya ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake nchini.

Hivyo, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kuimarisha uwajibikaji, weledi na uwazi katika kusimamia programu za kitaifa ili ziweze kufikia malengo makuu.

Aidha, alikiri kwamba tokea kuridhia utekelezaji wa kizazi chenye usawa na kuendelea vyema katika utekelezaji wa programu hiyo, lakini, bado kuna changamoto chache zinazopaswa kufanyiwa kazi ili ziwe na maono ya utekelezaji kwa kuzingatia Mpango kazi ambao kila taasisi inapaswa kuutekeleza.

Naibu Mwakilishi wa UN Women Tanzania, Catherine Gifford, alisema, UN Women inatambua umuhimu wa taasisi hizo katika kushughulikia uwepo wa usawa wa kijinsia zikiwa na uwezo wa kushawishi sera, kuunda kanuni za kijamii na kuwaandaa viongozi wajao kwa maarifa na dhana ya kukuza usawa wa kijinsia.

# Wafugaji wa Kizimkazi wachota mbinu Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA juhudi za kuimarisha sekta ya ufugaji na kuboresha ustawi wa jamii, kampuni ya Asas imetekeleza ahadi yake iliyoitoa kwa Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa sherehe za Kizimkazi Festival kwa kuandaa ziara ya wafugaji kutoka Kizimkazi kwenda kwenye mashamba yake ya mkoani Iringa.

Mnamo Agosti 8 mwaka huu, kampuni hiyo iliahidi kuwapa wafugaji wa Kizimkazi fursa ya kujifunza mbinu za kisasa za ufugaji katika mashamba yake.

Ofisa Masoko wa kampuni ya unywaji na uuzaji maziwa, Jimmy Kiwelu, alieleza mwishoni mwa wiki namna wafugaji wa Kimzikazi walivyopata elimu na fursa juu ya ufugaji.

"Kama utakumbuka kwenye sherehe za Kizimkazi Festival tuliahidi kuwaleta wafugaji wa Kizimkazi katika mashamba yetu na hatimaye tumetekeleza, na ziara hii kwa wafugaji hawa imetufungulia macho, na maarifa mapya ambayo yakitumika vizuri yatasadia kuongeza uzalishaji na kuboresha maisha yetu.

> **"Katika ziara hii, wafugaji wapatao 50 wamepata nafasi ya kushuhudia mifumo ya kisasa ya malisho, mbinu za matibabu ya mifugo na usindikaji maziwa," alisema.**

"Katika ziara hii, wafugaji wapatao 50 wamepata nafasi ya kushuhudia mifumo ya kisasa ya malisho, mbinu za matibabu ya mifugo na usindikaji maziwa," alisema.

Vilevile, ofisa huyo alisema wafugaji hao pia wamepata elimu juu ya jinsi ya kuboresha uzalishaji na kudumisha afya ya mifugo yao kwa njia endelevu.

"Kwa miaka mingi, tumekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono maendeleo ya kilimo na ufugaji, ikiwa ni sehemu ya mkakati wake wa uwajibikaji wa kijamii.

"Utekelezaji wa ahadi hii unadhihirisha dhamira ya dhati ya kusaidia wafugaji wadogo ili kuongeza kipato na kuboresha maisha yao," alisema.

Ziara hiyo, aliitaja Kiwelu ni mwanzo wa ushirikiano endelevu na inatarajiwa kuleta mabadiliko chanya kwa wafugaji wa Kizimkazi na maeneo mengine nchini.

Wakiwa katika mashamba hayo, wafugaji hao walisema sekta binafsi inaweza kuchangia maendeleo ya kijamii kwa vitendo kupitia uwekezaji katika elimu na mafunzo kwa jamii za wafugaji.

Walipongeza kampuni hiyo kwa kujizatiti kuendelea kushirikiana na wafugaji wa maeneo mbalimbali ili kuboresha sekta ya ufugaji nchini.




Makamu wa kwanza wa rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman akizungumza katika mkutano wa nne wa taasisi ya Maalim Seif Sharif Hamad uliofanyika leo visiwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Katibu Mkuu Kiongozi aeleza umuhimu wa sekta ya ujenzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi Zanzibar, Zeena Ahmed Said amesema sekta ya ujenzi ni muhimu kwa mustakbali wa nchi na fedha nyingi za serikali zinakwenda kwenye masuala ya ujenzi.

Amesema serikali ina jukumu la kutengeneza miundombinu ikiwemo barabara, maji, ujenzi wa hospitali, majengo katika sekta ya elimu na makazi. Zeena ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar alisema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi katika kujenga miundombinu, hivyo wasimamizi wa majengo wanapaswa kuacha kufanya udanganyifu ili kuepusha maafa ya majengo kuporomoka.

Aidha, aliwataka waingizaji wa vifaa vya ujenzi kuingiza vifaa vyenye ubora lakini makandarasi nao kujenga kwa mujibu wa ubora wa vifaa vilivyokubaliwa katika mikataba.

Pia, aliwataka makandarasi na wasambazaji vifaa vya ujenzi kuwa na ushirikiano ili kutengeneza timu ya kibiashara ili kupata miradi mikubwa na kupata fursa mbalimbali, huku akiwasisitiza kufanya kazi kwa uaminifu.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Makame Haji Makame alisema mafunzo hayo asili yake ni Sheria Namba 6 iliyoanzisha Bodi ya Wasajili ya Makandarasi ya Mwaka 2008, Kifungu 11(a).

Alisema kifungu hicho kinaainisha moja ya majukumu ya bodi ni kupanga na kutoa mafunzo juu ya masuala yanayohusiana na ujenzi ni sehemu ya maandalizi ya ufunguzi wa maabara mpya iliyopo chini ya taasisi ya ZBS.


Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar ambao umeelekeza kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya kisasa yenye viwango ili kuchochea maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

Alisema mafunzo hayo yamekuja na kauli mbiu isemayo ujenzi bora na salama ni wenye kuzingatia viwango ambapo lengo ni kuimarika ubora na usalama kwa watumiaji wa miundimbinu hiyo ambao kwa kiasi kikubwa utahakikisha maendeleo ya uchumi wa Zanzibar katika nyanja na miundombinu ya ujenzi wa kisasa iliyo imara na usalama wa wananchi.

Mrajisi wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Mansour Mohammed Kassim, alisema mafunzo hayo yalihusisha matukio makuu manne ikiwemo mdahalo ambao umejadili mambo mbalimbali ikiwemo ukosefu wa sera ya ujenzi Zanzibar.

Mengine ni upungufu wa udhibiti viwango kwa bidhaa za ujenzi zinazoingia, miradi ya ujenzi kutozingatia miundombinu ya baadaye, makato makubwa katika taasisi za kifedha na mfumuko wa bei wa bidhaa za ujenzi.

# Hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Exaudi Kigahe (wa nne kulia) na Balozi wa Kenya hapa nchini, Isaack Njenga (wa nne kushoto), wakiwaongoza baadhi ya viongozi kukata keki wakati wa hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: ZOTE: JUMANNE**



Balozi wa Kenya hapa nchini, Isaack Njenga (kulia), akizungumza na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, wakati wa hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam.



Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya The Guardian, Jackson Paul (kulia),Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe (kushoto), na Meneja Usambazaji wa Kampuni hiyo, Denis Ntaita, wakiingia kwenye ukumbi kuhudhuria hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaudi Kigahe (wa nne kulia) na Balozi wa Kenya hapa nchini, Isaack Njenga (kushoto), akisalimiana na Balozi wa Kenya hapa nchini, Isaack Njenga, wakati wa hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya Maofisa wa Ulinzi wakitoa heshima wakati nyimbo za taifa zikiimbwa katika hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya mabalozi wakiwa wameziwakilisha nchi zao katika hafla ya miaka 61 ya uhuru wa Kenya iliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Sare mpya kuwaongezea hamasa polisi nchini Kenya

**NAIRONI,** Kenya

RAIS wa Kenya William Ruto amesema sare mpya za Jeshi la Polisi zinakaribia kutolewa na kwamba hatua hiyo itakuwa ni sehemu ya juhudi za utawala wake katika kuboresha huduma ya polisi nchini humo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mipango Mikakati ya Huduma za Kitaifa za Polisi na Idara ya Jimbo 2023-2027, juzi Rais Ruto alielezea umuhimu wa sare hizo mpya, akisema zitawatia moyo maofisa na kuongeza ari yao ya ufanyaji kazi.

"Kama nilivyosema hapo awali, tutawashirikisha polisi wanaume na wanawake ili tuwe na sare zinazofaa, najua hilo limekubaliwa. Na kinachosubiriwa sasa ni sisi kujitokeza na kuhakikisha tunawaweka polisi wetu.

"Pia wanawake walio na sare, ambayo inawapa msukumo wa kufanya kazi na kusonga mbele, kwa hivyo tena, hilo ni jambo ambalo tutazindua," alisema.

Wakati huo huo, kiongozi huyo aliahidi kujitolea kwake katika mpango thabiti wa kisasa wa polisi, akieleza kuwa Shilingi za Kenya bilioni tisa, tayari zimetumika katika mpango huo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, huku kiasi cha ziada kikitengwa kwa ajili ya uboreshaji zaidi.

"Nilijitolea kwamba tutajihusisha na mpango wa kisasa wa huduma yetu ya polisi. Tayari katika miaka miwili iliyopita, tumetumia KSh bilioni tisa katika mpango wa kisasa. Pia tutatumia KSh. Bilioni 20, lakini kwa hakika, tutatumia KSh bilioni 28 kuboresha huduma zetu za polisi.

"Nina furaha sana kwamba baadhi ya vifaa tayari vimetolewa, vingine viko njiani na tunaanza kuhisi athari za uboreshaji wa polisi katika kuimarisha usalama kote nchini," Ruto alisema.

Pia Rais Ruto alipongeza uongozi wa polisi na maofisa mashinani, akitambua jukumu lao katika kulinda raia, mali na maisha.

Aliwahakikishia Wakenya kuwa mpango huo wa uboreshaji wa kisasa utakamilika ndani ya miaka miwili, na kuwapa maofisa zana za kisasa za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza za kiusalama ipasavyo.

Ilielezwa kuwa Kenya Kwanza inataka sare za polisi zibadilishwe, kwa sababu wakati wa kampeni za urais 2022, aliyekuwa naibu wa rais Rigathi Gachagua alisema hawatalegea katika kutekeleza mageuzi katika Huduma ya Kitaifa ya Polisi. **KTN**

# Afariki kwa kumwagiwa tindikali na mke wake

**NAIROBI,** Kenya

MWANAMUME wa miaka 52 wa Nakuru nchini Kenya amefariki kutokana na majeraha mabaya aliyoyapata baada ya mkewe kudaiwa kumshambulia kwa tindikali akiwa nyumbani kwake.

Mwanaume huyo aliyetambulika kwa jina la Elijah Matoke alidaiwa kumwagiwa tindikali juzi akiwa kitandani na kukimbizwa hospitalini na kufariki dunia alipokuwa akipatiwa matibabu.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari nchini humo mmoja wa mashuhuda Lilian Magomera ambaye ni jirani alisema alimsikia Matoke akipiga kelele baada ya kushambuliwa huku akihema kwa maumivu, na kwamba alikuwa akikikaribia kifo.

“Tulisikia kelele za ‘woi, ninakufa, wamenimaliza’ tulikuja hapa na tukamkuta akiwa na majeraha ya moto akiwa anaonekana rangi ya pinki, niliingiwa na hofu na kuwauliza watoto wake nini kimempata baba yao,” Lilian alisema.

Aliongeza kuwa watoto wa mwanaume huyo walimwambia kuwa hawakujua ni nani aliyemshambulia baba yao kwa tindikali.

Binti yake Claris Matoke alisema kwa uchungu kwamba baba yake alikufa kifo cha uchungu, akieleza kuwa alipata majeraha mabaya wakati wa kisa hicho.

"Nikiwa hospitalini, aliniita na kuniambia: "Binti yangu, nishike mkono unipeleke nyumbani." Sikujua ni nyumba gani anayozungumza kwa sababu hayo yalikuwa maneno yake ya mwisho," alisema huku akitokwa na machozi.

Kamanda wa Polisi wa Kaptembwa, Nakuru Magharibi, Anderson Njagi alithibitisha kisa hicho, akisema kuwa mke wa mwanamume huyo na mwanawe ndio washukiwa wakuu wa shambulio hilo.

"Wako rumande na tukimaliza uchunguzi, tutawafikisha mahakamani kwa kosa la mauaji," alisema Njagi.

Ilielezwa kuwa maelezo yanaonesha kuwa mshukiwa alikuwa ameolewa na marehemu kama mke wa pili kwa miaka 16. Walikuwa na mabishano ambayo yalizidi kuwa mashambulizi makali.

Pia inaelezwa kuwa wanandoa hao walikuwa na ndoa yenye matatizo. Na kwamba wakazi wa eneo hilo waliwashauri wanandoa hao kusuluhisha mizozo ya kinyumbani kwa amani badala ya kutumia nguvu za kimwili.

**KTN**



Mwanaume wa Syria akiendesha pikipiki yake akiwa amebeba familia yake, wakiwa wanayakimbia makazi yao yaliyoharibiwa kutokana na mashambulizi yaliyofanywa katika mji wa Harasta Mashariki nje kidogo ya Damascus jana. **PICHA: AFP**

## Idadi ya vifo yahofiwa kuongezeka Ufaransa

**MAYOTTE,** Ufaransa

MAOFISA wa Ufaransa wanahofia idadi ya vifo kuongezeka kutoka viwili vilivyorekodiwa awali baada ya Kimbunga Chido kupiga visiwa vya Mayotte, na kusababisha uharibifu wa miundombinu kwenye eneo lililoko karibu na Bahari ya Hindi.

Akizungumzia gharika hiyo jana Waziri Mkuu wa Ufaransa, Francois Bayrou, alisema kimbunga hicho kilichopiga eneo hilo kiliangamiza mitaa ya mabanda na kuharibu majengo ya serikali, hospitali na makazi ya muda.

Alisema hali hiyo imeibua wasiwasi kuhusu upatikanaji wa chakula, maji na usafi wa mazingira katika visiwa vya Bahari ya Hindi.

"Kila mtu anaelewa kuwa hiki kilikuwa kimbunga ambacho kilisababisha taharuki na vurugu ambayo haikutarajiwa," Bayrou alisema.

Aidha, ilielezwa kuwa Kimbunga Chido pia jana kilitarajiwa kupiga katika majimbo ya Cabo Delgado au Nampula Kaskazini mwa Msumbiji baada ya Mayotte.

Kaimu Waziri wa Mambo ya Ndani Bruno Retailleau aliongeza kuwa Kimbunga Chido kilisababisha maafa yasiyotarajiwa ikiwemo kuharibu njia zilizokuwa zikitegemewa.

"Itachukua siku kadhaa kubainisha idadi ya vifo, lakini tunaogopa kuwa inaweza kuwa kubwa," alisema.

Kimbunga hicho kilikuwa kimeweka eneo hilo katika hali ya tahadhari wakati kilipokaribia bara la Afrika, kikiambatana na upepo wa angalau kilomita 226 kwa saa (140mph).

Dhoruba hiyo pia ilipiga visiwa vya Comoro vilivyo karibu na kusababisha mafuriko na kuharibu nyumba.

Kaimu Waziri wa Uchukuzi Francois Durovray alisema kwenye X kwamba uwanja wa ndege wa Pamandzi wa Petite-Terre umepata uharibifu mkubwa. Huku wataalamu wa hali ya hewa wakisema kimbunga hicho ni cha karibu zaidi katika mfululizo wa dhoruba duniani.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) ilisema hali hiyo ilikuwa sawa na vimbunga vya Gombe mwaka 2022 na Freddy mwaka 2023, vilivyoua zaidi ya watu 60 na angalau 86 nchini Msumbiji.

Ilionya kuwa watu milioni 1.7 walikuwa hatarini, na kusema mabaki ya kimbunga hicho pia yanaweza kumwaga mvua kubwa katika nchi jirani ya Malawi, ambayo inaweza kusababisha mafuriko.

**ALJAZEERA**

## HABARI MICHEZO

# SINGIDA BS YAPANIA KUZISHUSHA SIMBA, YANGA LIGI KUU BARA LEO

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wowote itakaoupata Singida Black Stars leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Prisons, utaifanya kuzishusha timu za Simba na Yanga zilizo juu yake kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida ambayo ina pointi 27, ikipata ushindi leo itafikisha pointi 30 na kuipita Yanga iliyo nafasi ya tatu na pointi zake 27 na Simba yenye pointi 28 iliyo kwenye nafasi ya pili.

Katika mchezo huo utakaopigwa saa 8:00 mchana, Singida inahitaji kwa udi na uvumba ushindi huo ili ifikishe pointi 30 sawa na vinara wa Ligi Kuu, Azam FC.

Hata hivyo, ili iongoze msimamo wa ligi hiyo, Singida inahitaji ishinde mabao matano, kutokana na kuwa na tofauti ndogo ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Utakuwa ni mchezo wa 14 kwa Singida, huku Simba na Yanga zikiwa zimecheza michezo 11 kila moja.

Ofisa Habari wa Singida, Hussein Masanza, amesema wamejiandaa kikamilifu kwa mchezo huo ingawa wanafahamu hautokuwa rahisi kutokana na Prisons kuwa ni timu ngumu inapocheza kwenye uwanja wake wa nyumbani.

"Tuko Mbeya na wachezaji 24, ambao ndiyo baadhi yao wanatarajia kushuka dimbani, tunafahamu Prisons ikiwa nyumbani ni timu ngumu sana kwa hiyo tunajiandaa kisaikolojia pia, ingawa walimu wetu wanaendelea kuzungumza na wachezaji umuhimu wa mchezo huu, tunaamini kuwa maandalizi yanayoendelea kufanyika, tutafanya vizuri," alisema Masanza.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, David Ouma, alisema kuwa kwa sasa wanajaribu kuizoea hewa ya Mbeya, huku akisema wanafahamu aina ya soka ambalo Prisons wanacheza.

"Tutacheza kwa jinsi ambavyo wao watakuja, tunajua aina yao ya mpira wanavyocheza, lakini wakibadilika na sisi tutabadilika ili twende nao sawa, nadhani hayo yanaweza kutusaidia kupata ushindi," alisema Ouma.

Mbali na mechi hiyo, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, wenyeji, KMC, watakuwa dimbani kuwakaribisha Pamba Jiji, mechi itakayochezwa, saa 10:00 jioni.

**SHUTI...**




Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya, akiachia shuti huku kiungo mkabaji wa TP Mazembe, Josue Mungwengi, akihaha kumzuia kwenye mechi ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa juzi katika Uwanja wa TP Mazembe, Lubumbashi, DR Congo na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Namungo yathibitisha kumsajili Amoah

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Namungo FC, imetangaza rasmi kumsajili beki wa kati na kiungo mkabaji wa zamani wa Azam FC, Daniel Amoah.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa wana imani kuwa, Amoah ataongeza kitu kwenye kikosi hicho kutokana na uzoefu wake kwenye michezo ya ligi na kimataifa.

Siku chache zilizopita, gazeti ya Nipashe liliandika habari ya mchezaji huyo raia wa Ghana kuwa yupo kwenye mazungumzo wa viongozi wa Namungo kutokana na vyanzo vya habari kutoka ndani ya klabu hiyo kulieleza.

"Kama unavyoona hatujafanya vema sana karibuni mzunguko wote huu wa kwanza, kwa maana hiyo ni lazima tuongeze watu, Namungo hii si ile ambayo watu wanaijua, tunataka mzunguko wa pili tufanye marekebisho kadhaa, na kwa kuanzia, tunaanza upande wa ulinzi, tumezungumza na Amoah, yule ambaye alikuwa akiichezea Azam.

"Anacheza nafasi ya kiungo mkabaji, hata beki wa kati nadhani atatusaidia, huku tukiwa tunaangalia maeneo mengine. Tukishakamilisha kila kitu sasa ndiyo tutatoa taarifa rasmi kwa waandishi wa habari," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo kabla ya taarifa rasmi kutolewa jana.

Kiungo huyo aliingia nchini mwaka 2016, akisaijiliwa na Azam, kutokea Klabu ya Medeama ya Ghana, baada ya kuonekana kwenye mechi mbili za Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya Yanga.

Mechi ya kwanza iliyochezwa, Julai 16, 2016 nchini, Medeama na Yanga zilitoka sare ya bao 1-1, kabla ya Julai 26, mwaka huo, timu hiyo ya Ghana kushinda mabao 3-1, akionesha uwezo mkubwa kwenye mechi hizo, kiasi cha mabosi wa Azam kuvutiwa na kiwango chake na kumsajili.

Aliitumikia Azam kwa miaka minane kabla ya kuachwa mwishoni mwa msimu uliopita.

## Pamba yanasa beki kutoka Cameroon

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba Jiji, imetangaza kunasa saini ya beki wa pembeni, Cherif Ibrahim, kutoka Klabu ya Coton Sport FC ya Cameroon.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, pia imethibitisha rasmi kuwasajili wachezaji, Deus Kaseke, Habib Kyombo na Hamad Majimengi kwa ajili ya kuimarisha kikosi hicho kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa saa sita usiku wa kuamkia kesho.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, usajili huo na mwingine utakaotangazwa, ni mapendekezo ya bechi la ufundi chini ya Kocha Mkuu, Fred Felix Minziro.

"Tumesajili wachezaji hao na tutaendelea na usajili kwa matakwa ya benchi la ufundi kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chetu," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Cherif ni beki wa kushoto, Majimengi hucheza winga zote mbili, akiwa amecheza kwenye Klabu za Ruvu Shooting, JKU, Coastal Union, Namungo na Singida Black Stars huku Kyombo akiwa ni straika aliyewahi kuhudumu Klabu za Mbeya City, Mbeya Kwanza, Simba na Singida Black Stars.

Kwa upande wa Deus Kaseke ni winga mzoefu aliyewahi kuzichezea Klabu za Mbeya City, Yanga na Singida Big Stars na mpaka anajiunga na Pamba Jiji alikuwa hana timu yoyote.

"Nimefurahi sana kujiunga na timu hii, ina historia kubwa katika soka la Tanzania, mimi na wachezaji wenzangu tuliojiunga tunajua tumeletwa ili kuipambania timu itoke kwenye eneo ilipo sasa, tunaahidi kwa ushirikiano na mashabiki tutaiwezesha Pamba kufanya vizuri," alisema Kaseke.

Timu hiyo iko kwenye nafasi ya 12 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 12, ikicheza michezo 14 mpaka sasa.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inatazamia kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ufaransa, Paul Pogba, ambaye anatarajiwa kurejea uwanjani Machi baada ya kumaliza kifungo chake, lakini inaaminika kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United na Juventus mwenye umri wa miaka 31, anasita juu ya kukubali mpango huo wa City. (***Independent***)

### KUDUS AWA LULU

KLABU ya Newcastle United, Arsenal na Liverpool wapo kwenye mbio moja za kutaka kumsajili winga wa West Ham, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 24, lakini 'Magpies' watalazimika kuwauza baadhi ya wachezaji wao katika dirisha la usajili la Januari ili kupata fedha za kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ghana. (***Mirror***)

### ARNOLD HATAKI TENA

MLINZI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, anamaliza mkataba wake na klabu hiyo yenye maskani yake katika Uwanja wa Anfiled mwishoni mwa msimu huu na amesema hataruhusu mazungumzo na klabu kuhusu mkataba mpya "kujadiliwa hadharani". (***Sky Sports***)

### MADRID WAKOMAA NAYE

ALEXANDER-Arnold bado anasalia kuwa lengo kuu la usajili wa Real Madrid mwishoni mwa msimu. Miamba hiyo ya Hispania pia inataka kusajili beki mpya wa kati na kuongeza mkataba wa kipa wao namba moja, Thibaut Courtois, 32. (***Fabrizio Romano via Teamtalk***)

### AMORIM KUONGEZA NYOTA

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, analenga kufanya usajili wa beki mpya wa kushoto, mshambuliaji na kiungo mshambuliaji ili kuongeza uimara wa kikosi chake katika dirisha la usajili la Januari. (***Football Insider***)

### KANE HANA MBADALA

BAYERN Munich hawatatafuta mbadala wa mshambuliaji wao na nahodha wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 31, ambaye ameumia, kuelekea dirisha la usajili la Januari. (***Sky Sports Germany***)

### GORDON APUUZIA

NYOTA wa England, Anthony Gordon amepuuzilia mbali uvumi kuwa alitaka kuondoka Newcastle United baada ya msimu uliopita, kabla ya dili la kuhamia Liverpool kushindikana, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, akisema "anafuraha sana" kuwapo katika klabu hiyo yenye maskani yake pale St James' Park. (***Sky Sports***)

### FRIMPONG KURUDISHWA CITY

MANCHESTER City ina nia ya kumnunua tena beki wa pembeni wa Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 24, kutoka Bayer Leverkusen ikiwa ni miaka mitano baada ya kuondoka katika akademi yao na kujiunga na Celtic. (***Football Insider***)

### TISA TU HAWAUZWI UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, amesema ni wachezaji tisa tu katika kikosi chake ambao hawawezi kuuzwa, huku kiungo wa kati wa Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 30, na winga wa Argentina, Alejandro Garnacho (20), wakiwa miongoni mwa majina yaliyo katika hatari ya kuuzwa. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MCHEZAJI WA MAN CITY AUTWAA URAIS GEORGIA

**●●● Atangazwa kuwa rais wa nchi hiyo usiku wa kuamkia jana baada ya kuibuka kidedea katika...**

**TBILISI,** Georgia

MCHEZAJI wa zamani wa Klabu ya Manchester City ya Ligi Kuu England, Mikheil Kavelashvili, ametangazwa kuwa rais wa nchi ya Georgia usiku wa kuamkia jana Jumapili.

**Kavelashvili mwenye umri wa miaka 53, alikuwa mgombea pekee kwenye kinyang'anyiro hicho na alishinda kura kwa urahisi kutokana na udhibiti wa chama chake cha Georgian Dream chenye viti 300 am bacho pia kilichinda urais mwaka 2017.**

Kama ilivyo kwa wachezaji wengi mashuhuri wa Georgia, Kavelashvili alianza uchezaji wake katika Klabu ya Dinamo Tbilisi, akitokea kwenye academi ya vijana mwaka 1989.

Akiwa mshambuliaji mahiri, alijiimarisha katika pale Dinamo kabla ya kuhamia Klabu ya Urusi ya Spartak Vladikavkaz mwaka 1995.

Kavelashvili alianza mazoezi na Manchester City Machi Mosi, 1996, kabla ya kujiunga na klabu hiyo katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili.

Alianza kuichezea Man City kwa mara ya kwanza Aprili 6 akifunga bao kwenye mchezo wa dabi dhidi ya Manchester United.

Baada ya kushushwa daraja kwa City, alicheza michezo 24 (mabao mawili) na akapelekwa kwa mkopo Grasshoppers na kushinda Ligi Kuu ya Uswisi mwaka 1998.

Tangu wakati huo amecheza sehemu kubwa ya soka lake nchini Uswisi, akizichezea Zurich, Luzern, Sayuni na Aarau. Aarau walimtoa kwa mkopo Vladikavkaz 2004, lakini alirejea Uswisi baada ya kucheza mechi saba pekee.

Kavelashvili alijiunga na kikosi cha kwanza cha Basel katika msimu wao wa 2005-06 chini ya Kocha Mkuu, Christian Gross, ambaye alikuwa katika msimu wake wa saba na klabu hiyo.

Hapo alicheza kwa msimu moja na kustaafu rasmi soka la kulipwa.

Chana hicho ndio kinaunda wabunge, mabaraza ya manispaa na mikoa.

Chama cha Dream ya Georgia pia kilichukua udhibiti wa Bunge katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 26, mwaka huu.

Rais anayemaliza muda wake wa Georgia na vyama vikuu vya upinzani vilisusia uchaguzi huo wakitaka urudiwe huku kukiwa na madai kuwa uchaguzi huo ulivurugwa kwa usaidizi wa Urusi.

## Arteta ajitetea kumtoa Odegaard

**LONDON,** England


MIKEL Arteta ametetea uamuzi wake wa kumtoa nahodha, Martin Ødegaard katika suluhu ya Arsenal dhidi ya Everton kwenye Ligi Kuu England juzi, kwa kusisitiza kuwa ulikuwa "uamuzi wa kimbinu."

'Washikabunduki' hap walibanwa na kutoka suluhu kwenye Uwanja wa Emirates ambapo, licha ya kusaka bao, Arteta alichukua uamuzi wa kumtoa Odegaard dakika ya 62 na kumuingiza kinda Ethan Nwaneri.

Arsenal hawakuweza kutafuta njia ya kumpita mlinda mlango wa Everton, Jordan Pickford na wanaweza kuanguka kwa pointi nne nyuma ya Chelsea walio nafasi ya pili kama jana Jumapili waliwafunga Brentford.

"Kwa Martin ilikuwa uamuzi wa busara kujaribu kubadilisha mdundo wao upande huo," alisema Arteta.

"Ninaelewa. Ethan akiingia na kufunga bao, ni bao zuri sana. Asipofanya hivyo, umemtoa nahodha wako. Hiyo ni soka."



Odegaard alibadilishwa pamoja na Declan Rice, ambaye Arteta alifichua kuwa bado hana utimamu wa kimwili.

"Nikiwa na Declan ilibidi nimuondoe kwa sababu alikuwa anahisi kitu," alisema.

"Mwisho hii ni soka - jambo gumu zaidi ni kufanya kile tunachopaswa kufanya katika dakika hizo 20 hadi 25 za mwisho.

"Sifa kwao pia, jinsi walivyojilinda, jinsi walivyozuia michomo, hongera kwa Pickford aliokoa hatari nyingi."



# REAL MADRID WALIA KUNYIMWA PENALTI

**VALLECAS,** Hispania

REAL Madrid wamelalamikia kitendo cha mwamuzi kushindwa kuwapa penalti katika sare ya mabao 3-3 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La-Liga, dhidi ya Rayo Vallecano Jumamosi, na kuitaja kuwa "mechi ambayo tungeweza kushinda."

Madrid ilikuwa nyuma kwa mabao 2-0 mjini Vallecas kwa mabao ya mapema ya Unai Lopez na Abdul Mumin wa Rayo, kabla ya Federico Valverde na Jude Bellingham kusawazisha na kufanya matokeo kuwa 2-2.

Halafu Rodrygo akaiweka mbele Real Madrid kipindi cha pili na Isi Palazon akaisawazishia Rayo dakika nane baadaye na mchezo kumalizika kwa sare. Na sasa wamewaacha Barcelona kwa pointi moja kileleni kabla ya mchezo wa jana, Jumapili.

Baada ya mchezo huo, wababe hao wa LaLiga walitoa ripoti ya mechi yenye kichwa cha habari "Mwamuzi mwenye utata amewanyima ushindi Madrid" kwenye mitandao yao ya kijamii na kwenye tovuti ya klabu hiyo, na kushambulia uamuzi wa mwamuzi Juan Martinez Munuera wa kutotoa penalti baada ya Mumin kuonekana akimchezea madhambi Vinicius Junior kipindi cha pili.

"Katika dakika ya 75 ulikuja mchezo wenye utata zaidi wa mechi," ilisema ripoti hiyo.

"Vini aliangushwa ndani ya eneo la hatari na Mumin, lakini Martinez Munuera hakutoa penalti, wala hapakuwa na onyo lolote kutoka kwa Pablo Gonzalez Fuertes (mwamuzi wa VAR)."

Mara kwa mara Madrid wamekosoa uchezeshaji wa waamuzi msimu huu, wakitangaza kwenye kituo cha televisheni cha klabu, Real Madrid TV, wakionesha makosa ya waamuzi.

"Nilipoona marudio, penalti ilionekana wazi kwangu," alisema kocha Carlo Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, huku akisifia uchezaji wa timu yake kwa ujumla.

"Sare na Mallorca na Las Palmas Agosti zilikuwa tofauti kabisa na droo hii... Tuko kwenye njia sahihi."

"Sare za Mallorca na Las Palmas zilinifanya niwe na wasiwasi, lakini hii haikuwa hivyo," aliongeza Ancelotti.

"Nilidhani itakuwa vigumu sana kwetu kupata uwiano na mtazamo msimu huu, lakini tumeipata.

"Rodrygo alirejea leo (juzi). Eduardo Camavinga alirejea. David Alaba atarudi. Nitaanza 2025 kwa shauku kubwa na tuko tayari katika kupigania kila kitu."

Ancelotti alidokeza kwamba Madrid walianza dhidi ya Rayo kwa kuwakosa wachezaji muhimu wa kikosi cha kwanza kutokana na majeraha, akiwamo Kylian Mbappe, Ferland Mendy, Eder Militão na Dani Carvajal, huku Vinicius akianzia benchi.

"[Viniciu] hakuanza kwa sababu hajacheza dakika 90 tangu apone jeraha lake," alisema Ancelotti.

"Tulipendelea acheze kipindi cha pili, ambacho kinaweza kuwa kidogo. Alikuwa na mchezo mzuri."

Madrid watacheza Jumatano dhidi ya Pachuca katika fainali ya Kombe la Klabu Bingwa Dunia la FIFA.

# Slot aridhika matokeo Liverpool



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, amesema hangeweza kutaka zaidi kutoka kwa wachezaji wake baada ya sare ya mabao 2-2 na Fulham kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi, hasa baada ya kubakiwa na wachezaji 10 uwanjani.

Liverpool walimaliza mchezo huo wakiwa na wachezaji 10 baada ya Andy Robertson kuoneshwa kadi nyekundu.

Liverpool wamebakia kileleni kwa pointi 36, tano mbele ya Chelsea, ambao jana Jumapili walikuwa wakiwakaribisha Brentford na sita mbele ya Arsenal, ambao walitoka suluhu na Everton juzi.

Andreas Pereira aliiweka Fulham mbele dakika ya 11 akiunganisha pasi ya Antonee Robinson na kumpita beki wa pembeni wa Liverpool, Andy Robertson na kumtungua kipa Alisson.

Robertson alioneshwa kadi nyekundu dakika sita baadaye kwa kumchezea vibaya Harry Wilson kabla ya Cody Gakpo kusawazisha dakika mbili baada ya kipindi cha mapumziko akiunganisha kwa kichwa krosi ya Mohamed Salah.

Lakini Rodrigo Muniz akaiweka tena mbele Fulham dakika ya 76 alipounganisha krosi ya Robinson iliyomgonga Alisson na kujaa wavuni.

Jota ambaye alikuwa akicheza mchezo wake wa kwanza tangu kuumia dhidi ya Chelsea Oktoba, alimfunga Bernd Leno dakika ya 86 huku Liverpool wakiepuka kile ambacho kingekuwa kipigo cha pili kwa Slot katika michezo 23 kwenye mashindano yote.

"Singeweza kutaka zaidi kwa wachezaji," alisema Slot baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Sidhani kama ningeomba zaidi kutoka kwa wachezaji wangu, haswa baada ya kuwa na wachezaji 10."

## Mazembe yampa kiburi Ramovic

INATOKA UKURASA 24

ushindi.

Yanga ilimiliki zaidi mchezo kipindi cha pili hasa baada ya kufanya mabadiliko kadhaa ya wachezaji, Dube aliyechukua nafasi ya Kennedy Musonda, Stephane Aziz Ki, aliyeingia badala ya Maxi Nzengeli, Clement Mzize, aliyeingia badala ya Mudathir Yahaya, na Clatous Chama aliyechukua nafasi ya Duke Abuya.

Hata hivyo, pamoja na ushindi huo, bado Yanga inaburuza mkia ikiwa na pointi moja, TP Mazembe ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake mbili.

Timu ya Al Hilal Omdurman inaliongoza Kundi A, ikiwa na pointi tisa, baada ya juzi usiku kupata ushindi wa bao 1-0 ikiwa ugenini, Uwanja wa Julai 5 nchini Algeria, dhidi ya MC Alger, bao lililofungwa na Guessouma Fofana dakika ya 76.

Al Hilal imeshinda michezo yake yote mitatu iliyocheza, huku MC Alger ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne mpaka sasa.

Wakati hayo yakiendelea kocha huyo amesema sasa anarejea kwenye michezo ya Ligi Kuu, akisema anakuja na mfumo tofauti na aliowaelekeza wachezaji wake dhidi ya TP Mazembe.

Alisema anafanya hivyo kwa sababu kwenye Ligi Kuu timu zinacheza tofauti na michezo ya kimataifa inavyochezwa.

"Huku unaweza kupata nafasi ya kumiliki mpira wakati mwingine bila kubugudhiwa, kwenye Ligi Kuu timu nyingi zinakabia chini na hazitoi nafasi, nakwenda kutengeneza mpango mkakati wa kucheza aina hizo za mechi, hatuwezi kucheza kama hivi tulivyocheza na TP Mazembe," alisema kocha huyo.

Yanga inatarajia kurejea kwenye mechi za Ligi Kuu, Alhamisi wiki hii itakapocheza dhidi ya Mashujaa FC, mechi inayotarajiwa kupigwa, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

# RUPIA YUKO TAYARI KUTUA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

KINARA wa mabao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Elvis Rupia, amesema atakuwa tayari kujiunga na Simba kama kweli wanamhitaji na watapitia kwenye njia sahihi za kuongea na klabu yake ya Singida Black Stars, kwani hakuna mchezaji yeyote nchini ambaye hataki kuichezea timu hiyo.

Rupia, raia wa Kenya, alisema hayo juzi kutokana na tetesi kuwa Klabu ya Simba inataka saini yake kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

"Mpaka sasa binafsi sijapata ofa kutoka klabu yeyote, labda inaweza kuja baadaye, ukweli hakuna mchezaji yeyote nchini ambaye haipendi kucheza Simba au Yanga, ikitokea ofa na nikakubaliana nayo naweza kwenda," alisema mchezaji huyo.

Habari kutoka ndani ya Klabu ya Simba zinasema kuwa inamhitaji mchezaji huyo kwa ajili kuongeza nguvu kwenye kikosi cha timu hiyo nafasi ya ushambuliaji ambayo ina Leonel Ateba, Steven Mukwala na Valentino Mashaka.

Hata hivyo, wakati Simba ikionesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo, habari zinasema kuwa Yanga nayo ina mpango wa kupiga hodi kwenye klabu hiyo kuulizia huduma ya mchezaji huyo ambaye amefikisha jumla ya mabao saba ya kufunga kwenye Ligi Kuu, akimpiku straika wa Fountain Gate, Selemani Mwalimu, aliyeongoza kwa muda mrefu akisalia na mabao sita.

Akizungumzia siri ya kupachika mabao, Rupia alisema ni kufanya mazoezi kwa bidii na amejiwekea malengo ya kufunga bao moja katika kila mechi, ingawa baadhi ya michezo ameshindwa kufanya hivyo.

"Kulingana na jinsi ninavyofanya mazoezi, nimekuwa nikijiwekea malengo angalau nifunge bao moja kila mchezo, ila kuna wakati haitokei, nashukuru kwenye mchezo dhidi ya Dodoma Jiji nimefunga mabao yote mawili nikaipa ushindi timu yangu ya mabao 2-1, sikujua kama nitafunga mawili, moja limeongezeka.

"Ni furaha sana kwa sababu kila straika anataka kuwa hapo juu, kila mmoja anapambana anavyoweza aweze kufika hapo.

"Binafsi natarajia kuendelea kufunga mabao mengi, huko mbele ndiyo tutajua ni nani atakuwa mfungaji bora," alisema Rupia.

KOKOTA...



Beki wa kushoto wa Simba, Valentin Nouma, akikokota mpira huku akipata upinzani kutoka kwa mchezaji wa CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU**

## Tisa za Ligi Kuu, 10 Championship zatinga raundi ya nne Kombe la FA

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya timu tisa za Ligi Kuu na 10 za Ligi ya Championship zimetinga hatua ya raundi ya nne ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), maarufu Kombe la FA zilizochezwa wiki iliyomalizika kwa siku tano mfululizo.

Jumla ya michezo 19 imechezwa, kasoro timu za Simba na Yanga ambazo zipo kwenye hekaheka ya michezo ya kimataifa.

Mechi hizo ni za kusaka ubingwa kwa ajili ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Tukianza na timu 10 za Championship zilizotinga raundi nne ni Transit Camp, iliyoifunga Gunners mabao 3-2, mechi ikichezwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, Biashara United ikiitandika TRA mabao 5-0, mchezo uliopigwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Songea United nayo ilipata ushindi kwa mikwaju ya penalti 3-2 dhidi ya Kidulu FC, baada ya sare ya mabao 2-2 katika Uwanja wa Majimaji, Songea, Cosmopolitan ikishinda 2-0 dhidi ya Nyota FC Uwanja wa Mabatini, Polisi Tanzania ikaidundua Bukombe FC, bao 1-0, Uwanja wa Ushirika, Moshi.

Stand United pia iliichapa Don Bosco mabao 2-0, Uwanja wa Kambarage, Mbeya City ikaifunga Mapinduzi, mabao 2-1, Uwanja wa Sokoine, Mbeya, Green Warriors ikaichapa Hausung kwa penalti 4-2, baada ya sare ya bao 1-1, Mabatini, na TMA, ikaiangamiza Leopards FC mabao 5-1, Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kwa upande wa timu za Ligi Kuu, Singida Black Stars ilishinda 2-0 dhidi ya Magnet katika Uwanja wa Liti mkoani Singida, Mashujaa ikaitwanga Tukuyu Stars, mabao 3-0 Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, Pamba ikashinda bao 1-0, dhidi ya Moro Kids, CCm Kirumba jijini Mwanza, Coastal Union ikashinda 4-0 dhidi ya Stand FC Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Azam nayo ikaifunga Iringa Sports mabao 4-0 Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Namungo ikashinda 2-1 dhidi ya Tanesco FC, Majaliwa, Ruwanga mkoani Lindi, JKT Tanzania ikipata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Igunga, Uwanja wa Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

## *Simba hatari kwa Mkapa mechi CAF*

INATOKA UKURASA 24

ni Joshua Mutale aliyechukua nafasi ya Ahoua, Kagoma, akichukua nafasi ya Debora Fernandes Mavambo, Steven Mukwala aliyetwaa nafasi ya Ateba, Chamou Karaboue, akichukua nafasi ya Che Malone, na Valentin Nouma ambaye aliingia nafasi ya Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Baada ya ushindi huo, Simba imepanda hadi nafasi ya pili nyuma ya CS Constantine ya Algeria, ikifikisha jumla ya pointi sita sawa na vinara hao ambao jana usiku walitarajia kucheza nchini Angola dhidi ya Bravo do Maquis ambayo ilishuka hadi nafasi ya tatu, huku Watunisia hao wakibaki mkiani wakiwa hawana pointi, wao na Simba wakicheza michezo mitatu.

Katika mchezo wa jana, Simba itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kuwa mbele dakika 45 za mwanzo licha ya kumiliki mpira kutokana na wachezaji wake kutocheza kwa kasi, badala yake walikuwa wakicheza taratibu na pasi fupi fupi zisizokuwa na maana yoyote.

Ateba alipigwa kichwa kilichotoka nje akiunganisha krosi ya Awesu Awesu dakika ya 26, lakini pia akishindwa kukwamisha mpira wavuni dakika ya 33 na 34.

Dakika moja kabla ya mpira kumalizika, golikipa wa Simba, Camara, alifanya kazi ya ziada, alipochupa na kupangua shuti kali la Habessi Achref, ambaye alipigiwa mpira mrefu kutoka nyuma na kufanya shambulizi la kushtukiza.

Kabla ya kuingia kwa bao la ushindi, Simba ilikosa mabao dakika ya 89 kupitia kwa Joshua Mutale, shuti lake likipanguliwa na kipa Aymen, na dakika tatu baadaye Shomari Kapombe nusura afunge bao, lakini kipa huyo alikaa imara na kuokoa.

# Michezo

Nipashe Jumatatu Desemba16, 2024




Mchezaji wa Man City autwaa urais Georgia UKURASA 21

ASANTE MSWEDEN...



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akiifungia timu yake bao la kusawazisha dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 2-1. Mabao yote ya Simba yalifungwa kwa kichwa na Kibu. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba hatari kwa Mkapa mechi CAF

## ●●● Kibu shujaa wa mchezo, atupia mawili, mashabiki CS Sfaxien waking'oa viti baada ya...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya nane ya nyongeza lililofungwa na winga, Denis Kibu, liliiwezesha Simba kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mchezo wa Kundi A raundi ya tatu, Kombe la Shirikisho Afrika, uliochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kuendeleza rekodi yake nzuri inapocheza kwenye dimba hilo mechi za kimataifa.

Wakati mashabiki wote waliokuwa uwanjani hapo wakidhani mechi hiyo ingemalizika kwa sare ya bao 1-1, pasi ndefu iliyopigwa na Yusuph Kagoma, ikamkuta Kibu ambaye alipiga kichwa cha kiufundi, mpira ukionekana kama unatoka nje, huku kipa Aymen Dahmen akiwa anautazama tu, mpira ukakwama ndani ya wavu na kuibua shangwe na hoi hoi kutoka kwa mashabiki wa Simba.

Kwa hasira, mashabiki wachache wa timu hiyo ya Tunisia walianza kung'oa viti vya uwanjani hapo na kuvitupa chini, huku wachezaji na viongozi wa timu hiyo wakienda kuwavaa waamuzi kwa madai kuwa wamezidisha muda.

Hata hivyo, kwa muda mrefu wachezaji wa CS Sfaxien walionekana kupoteza muda mara kwa mara kitu ambacho kilisababisha mwamuzi kuzifidia.

Katika mchezo huo, mabao yote ya Simba yalifungwa kwa kichwa na Kibu, katika kila kipindi.

Bao la kwanza alilifunga dakika ya saba ya mchezo akiunganisha faulo iliyopigwa kwenye wingi ya kulia na Jean Charles Ahoua iliyomkuta mfungaji na kuruka juu kuukwamisha wavuni bila kukabwa na mchezaji yoyote wa CS Sfaxien, huku mabeki wake macho yao yakiwa kwa Leonel Ateba.

Bao hilo lilikuwa ni la kusawazisha baada ya kushtukizwa kwa bao la dakika ya tatu ya mchezo, likipachikwa na Hazem Haj Nassem kutokana na makosa ya beki Che Fondoh Malone.

Beki huyo akiwa ameumiliki mpira kwenye wingi ya kushoto, alitaka kumrudishia kipa wake Moussa Camara, lakini haukwenda mbali, badala yake straika huyo aliuwahi na kuukwamisha wavuni, licha ya juhudi za kipa kutokea kutaka kuuzuia.

Bao hilo lilionekana kuwashtua si wachezaji tu, bali hata mashabiki waliokuwa uwanjani, kwa bahati nzuri iliwachukua dakika nne tu Simba kusawazisha.

Simba ilionekana kuamka na kucheza kwa kasi dakika tano za mwisho na za nyongeza ambapo ni wao wenyewe tu walikuwa wakikosa mabao.

Kuingia kwa baadhi ya wachezaji kipindi cha pili kulionekana kuiamsha, baada ya kucheza kwa kasi ya chini kipindi cha kwanza.

Wachezaji walioingia kipindi cha pili

INAENDELEA UK. 23

# Mazembe yampa kiburi Ramovic

**Na Adam Fungamwago**

BAADA ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya TP Mazembe, ikirudisha bao dakika za majeruhi, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema mechi ya juzi ilikuwa ndiyo bora zaidi kucheza kwa kiwango kizuri kwa siku za karibuni, akizionya timu za Ligi Kuu kuwa dawa yao ipo jikoni.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya raundi ya tatu ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatua ya makundi, uliochezwa Uwanja wa Mazembe uliopo Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasin ya Congo, kocha huyo alisema timu yake ingeweza kushinda hata mabao matatu au manne kutokana na nafasi zilizotengenezwa, lakini walishindwa kuzitumia.

"Tangu nimefika Yanga nadhani huu ndiyo mchezo wetu bora zaidi kuwahi kucheza, tulifanya vitu vingi kwa usahihi na tulimsoma vema mpinzani, nadhani tulipaswa kufunga mabao matatu au manne kwa nafasi tulizotengeneza.

Tulimiliki mchezo, nimefurahi kwa hiki kilichofanyika, wapinzani wetu walituachia nafasi ya kuchukua mpira katikati bila upinzani, lakini pasi za mwisho nyingi hazikuwa sahihi, na chache zilizokuwa sahihi hazikutumika, inabidi kuboreshe hili, nawapongeza wapinzani kwa kutupa mechi nzuri," alisema kocha huyo ambaye ni mchezo wake wa tatu kuiongoza Yanga kwenye michezo ya kimataifa.

Katika mchezo huo, bao la TP Mazembe lilifungwa na Cheick Fofana dakika ya 42, kabla ya Dube kusawazisha dakika za majeruhi wakati mashabiki wa timu mwenyeji wakiwa wanaamini kuwa timu yao ingeibuka na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >